SUPA JACKPOT
TZS. 1,025,118,259
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**RAIS** Samia azijibu hoja mbili za CAG




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Agosti 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581050

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Makarani sensa kukatwa posho

**MTAKWIMU** Mkuu atoa angalizo kiutendaji... *Endelea ukurasa wa 2*



Wakili anayewatetea wabunge wa viti maalum 19 waliovuliwa uanachama na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ipilinga Panya (kushoto), akizungumza na wateja wake baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kuahirisha shauri lao jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sarakasi zaendelea kesi ya kina Mdee

UKURASA 2



UKURASA WA 3

## BUNGE LAINGILIA MKATABA NFRA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imebaini kusuasua kwa mradi wa ujenzi wa maghala ya hifadhi ya chakula na kuagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kukamilisha...

UKURASA WA 4

## TRA YATOA UFAFANUZI UTOZAJI KODI YA PANGO



MAMLAKA ya Mapato (TRA) imesema kodi ya pango siyo...

UKURASA WA 4

## MSAKO VIFUNGASHIO VYA PLASTIKI SASA NCHI NZIMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ametangaza kuanza kwa operesheni kabambe ya kutokomeza vifungashio vya plastiki ambavyo vimegeuka kuwa vibebeo Agosti 29, mwaka huu kwenye mikoa yote nchini...

# Matumizi ya fedha za NHIF yashtua

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC YAPEWA DOZI YA STAMINA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mjumbe wa Sensa kutoka nchini Marekani, Savy Surumpudi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu uwepo wa waangalizi wa sensa kimataifa ili kuangalia jinsi inavyofanyika. Kulia ni Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sarakasi zaendelea kesi ya kina Mdee

**Na Grace Gurisha**

WAKATI ilitarajiwa Mbunge wa Viti Maalum Halima Mdee na wenzake saba wangeanza kuhojiwa mahakamani jana, jopo la mawakili watano la wabunge hao limewasilisha hoja na kuilazimu mahakama kusubiri hadi Septemba 2, mwaka huu itakapotoa uamuzi ama wahojiwe au la.

Jana jopo hilo la mawakili wa kina Mdee lilidai mahakamani kwamba kabla ya kuhojiwa kwa wabunge wanane, yasikilizwe kwanza mapingamizi ya kiapo kinzani kilichowasilishwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), likidai kina upungufu wa kisheria.

Wabunge waliotakiwa kuhojiwa jana na mawakili wa CHADEMA ni Mdee, Grace Tendega, Esther Matiko, Esther Bulaya, Cecilia Pareso, Hawa Mwaifunga, Jesca Kishoa na Nusrat Hanje.

Mwenyekiti wa jopo hilo, Wakili Ipilinga Panya, aliomba jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu Masjala Kuu kuwa ibadilishe utaratibu wa usikilizwaji wa shauri hilo ili itoe nafasi ya hoja za kisheria kusikilizwa kwanza kama ilivyotakwa la kisheria.

Alidai kuwa baada ya kupokea kiapo kinzani kutoka CHADEMA, wamegundua kuna tatizo la kisheria kwamba kiapo hicho kina dosari za kisheria ambazo zitaweza kuleta athari kama shauri hilo litaendelea na usikilizwaji.

Panya alidai kwamba kiapo hicho kilipaswa kuwasilishwa na Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA iliyosajiliwa kwa sababu ndiyo waliyoishtaki na siyo vinginevyo.

Kutokana na dosari hizo, Wakili Panya aliomba wabunge hao wasihojiwe kwanza hadi mapingamizi yao ya kisheria yatakaposikilizwa kwa kuwa kuwapo kasoro hizo ni sawa na kwamba CHADEMA hajawasilisha kiapo kinzani kama amri ya mahakama ilivyoelekeza.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa CHADEMA, Peter Kibatala, pamoja na mambo mengine, alipinga ombi hilo na kusema walipaswa waombe marejeo ya mahakama kuhusu amri ilizozitoa Julai 29, 2022.

Wakili Kibatala alidai mahakama ilishatoa amri ya kuwa wabunge hao wanane waletwe na hivyo imefungwa mikono, iendelee na amri yake iliyotoa awali na kwamba amri hiyo haihusiani na uwasilishwaji wa kiapo kinzani.

Wakili Kibatala aliiomba mahakama itupe maombi hayo kwa gharama na pia waendelee na utaratibu uliopangwa na mahakama wa kuwahoji wabunge hao wanane.

Katika majibu yao, wajibu maombi wa pili na watatu (Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), kupitia Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola, walidai hawajawasilisha kiapo kinzani kwa kuwa hakuna malalamiko dhidi yao.

Mahakama baada ya kusikiliza mabishano hayo, ilipanga kutoa uamuzi wa jambo hilo Septemba 2, 2022 kama isikilize kwanza mapingamizi ya Mdee na wenzake au iendelee na utaratibu wa kuhojiwa kwa wabunge hao.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kusikiliza.

Pia wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na NEC kuchukua hatua yoyote dhidi yao hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Pamoja na mambo mengine, wabunge hao wanadai mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama haukuzingatia matakwa ya kisheria na misingi ya haki, wakidai hawakupewa haki ya kusikilizwa.

**ILIVYOKUWA KORTINI**

Nipashe ilishuhudia Mdee na wenzake wakifika eneo la mahakama kabla ya saa tatu asubuhi na walipowasili waliketi sehemu ya kusubiri mashauri kuitwa kuingia mahakamani.

Huku wakilindwa na walinzi watatu, mmoja akiwa amevaa suti nyeusi na ndani shati jeupe na tai na hao wengine walikuwa wamevaa suruali nyeusi, fulana nyeusi, mawani yenye rangi nyeusi na buti nyesi, wabunge hao walionekana wakisindikizwa na kulindwa na watu hao kila wanapokwenda.

Jinsi muda ulivyokuwa unakwenda, ndivyo idadi ya wafuasi wa CHADEMA ilivyoongezeka wakiwa wamevaa sare za chama hicho na ilipotimu saa 4:30 asubuhi, kulionekana kuwa na idadi kubwa ya wafuasi wa chama hicho kwenye viunga vya mahakama.

Ilipotimu saa 5:00 asubuhi, shauri lao liliitwa na kulikuwa na idadi kubwa ya watu na wengine walilazimika kusimama wakiwamo Mdee na wenzake, baadhi wafuasi hao waliombwa watoke katika benchi ili wabunge hao waketi, lakini waligoma kuwapisha.

Mmoja wa mawakili aliwaomba wanafunzi wa sheria waliokuwa katika mafunzo kwa vitendo kortini huko, wawapishe wabunge hao ili waketi, ndipo wakapata wasaa huo na ilipotimu saa 5:05 asubuhi, jaji aliingia mahakamani na shauri likaanza kusikilizwa.

Shauri hilo lilisikilizwa hadi saa 6:36 mchana na lilipoahirishwa, baadhi ya wafuasi wa CHADEMA, hasa wa jinsi ya kike, walisikika wakiwazomea Mdee na wenzake, lakini waleta maombi hao hawakujali, wakiingia kwenye magari yao na kuondoka.

# Makarani sensa kukatwa posho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitalipa posho kwa karani yeyote wa sensa atakayebainika kuandikisha kaya chini ya 100 kwa maeneo ya vijijini na 150 kwa mijini kulingana na mkataba wao.

Pia, imebainisha kuwa hadi jana, asilimia 54 ya Watanzania walikuwa wamehesabiwa kwenye sensa hiyo iliyoanza Jumanne ya wiki hii.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu Tanzania (NBS), na Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema kwa mujibu wa mikataba waliyoingia makarani na NBS, ni lazima kila mmoja ahesabu kuanzia kaya 100 hadi 150.

"Kama atafanya chini ya kiwango hicho, inamaana atakuwa hajafikia lengo tuliloweka na kama kuna karani yeyote amemaliza eneo lake alilopangiwa na hajafikisha idadi ya kaya hizo 100 hadi 150, tutaendelea kushikilia posho yake ya mwisho ambayo tulisema tutaitoa akikamilisha kaya hizo.

"Karani asikae akabweteka kuwa eneo lake la kuhesabia ni kaya 50 au 60, hapana! Tulishasema kama eneo lina kaya pungufu ya hizo, atatakiwa kwenda kuhesabu kaya zingine eneo lingine na hadi kutimiza ile idadi katika ile kata au eneo lingine ili kuhakikisha watu wote wanahesabiwa," alifanunua.

Alisisitiza makarani ambao hawatahesabu kaya kwa kiwango hicho, hawatalipwa na wahakikishe watu wote wanahesabiwa kwa kuwa hawataraji kuona sensa inafanyika chini ya malengo yaliyokusudiwa.

Mkurugenzi huyo alivipongeza vyombo vya habari kwa kuhamasisha vyema wananchi kwenye sensa hiyo kulinganisha na miaka ya nyuma.

Mjumbe kutoka Ofisi ya Sensa ya Marekani, Savy Surumpudi, alisema kazi hiyo ya sensa nchini imefanyika vizuri na wanatarajia malengo yatakayowekwa yatafikiwa.

"Tumeridhika mnakwenda vizuri kwa mujibu wa miongozo mliyotakiwa kufanya, tunafurahi kusaidia kazi hii," alisema.

Sensa hiyo ni ya saba kufanyika nchini, Tanzania ikiweka utaratibu wa kufanya sensa kila baada ya miaka 10.

## RIPOTI ZA CAG

# Bunge lashtuka matumizi makubwa ya fedha NHIF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imesema matumizi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ni makubwa kuliko mapato, hivyo na kushauri mfuko kuongeza wanachama ili kutotishia uhai wake.

Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kamati hiyo kukutana na viongozi na watendaji wa mfuko huo.

Alisema kamati hiyo imepokea taarifa ya uwekezaji, hesabu za mfuko na kupitia ushauri wa kisheria.

"Kamati imeitaka NHIF kuendelea kufanya mchakato wa kuongeza wanachama kwa sababu ukiangalia hesabu za NHIF unaona matumizi, yaani malipo ya huduma za wanachama zinavyoongezeka ikilinganishwa na mapato yake yanavyoongezeka.

"Kwa hiyo gharama zinaongezeka kuliko mapato, hivyo inahatarisha uhai wa mfuko. Kamati imeelekeza NHIF ifanye jitihada za makusudi za kuongeza wanachama na NHIF ifanye utaratibu wa kudhibiti matumizi," alisema na kuongeza kuwa kamati pia imeelekeza NHIF kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

"Kwa sababu mambo mengi yanayolalamikiwa na wanachama na yanayofanywa hata hivi majuzi taratibu zilizofanywa na kusitishwa na Waziri wa Afya, unaona kuna mapungufu (upungufu) ya (wa) mifumo hiyo," alisema.

Alisema kamati imeona kama NHIF itaimarisha mifumo yake kwenye majukumu yake yote kuanzia uandikishaji wanachama, utoaji huduma hadi madai ya watoa huduma yawe kwenye mfumo inayosomana.

"Tunaamini matumizi ambayo yanaonekana kuwa na aina fulani ya udanganyifu yatapungua, lakini vile vile na mapato yataongezeka ili mfuko uhudumie wanachama wake vyema hasa ikizingatiwa serikali ipo kwenye mchakato wa bima ya afya kwa wote," alisema.

Katika hatua nyingine, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuandaa mpango kazi ndani ya siku 30 wa namna ilivyojipanga kukabiliana na hoja za ukaguzi zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alisema mpango huo unapaswa kuwasilishwa kwenye kamati hiyo ili kuona utekelezaji wake.

"Tumeagiza mifumo yote ya ukusanyaji wa mapato ya serikali ionane, ifikapo Juni 30, mwaka 2023," alisema.

Alibainisha kuwa hoja zinazotakiwa kutengenezewa mpango kazi zinatokana na mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya forodha.

"Unakuta mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani hauonani na mfumo wa makusanyo wa forodha au mingine, ikiwa haionani huwezi kuwa na taarifa timilifu," alisema.

# Samia azijibu hoja za CAG

**Na Romana Mallya**



SERIKALI imeendelea kufanyia kazi hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) baada ya juzi usiku Rais Samia Suluhu Hassan (pichani) kuteua wenyeviti tisa wa bodi za taasisi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu, CAG Charles Kichere, mbali na mambo mengine, aliibua hoja ya mashirika na taasisi kadhaa za umma kutokuwa na bodi na watendaji wake kukaimu nafasi hizo kwa muda mrefu.

CAG Kichere katika hilo, ana angalizo kwamba taasisi na mashirika hayo kutokuwa na bodi kunaziweka hatarini fedha za umma katika mashirika na taasisi hizo, pia kukosekana ufanisi wa kiutendaji.

Kwa mujibu wa taarifa ilizotolewa juzi usiku, Rais Samia amefanya uteuzi wa wenyeviti wa bodi za taasisi hizo, pia Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Kamishna Mkuu wa Jeshi la Magereza.

Rais Samia amemteua Filbert Mponzi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Sukari Tanzania (SBT). Mponzi ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Dar es Salaam.

Wengine ni Ofisa Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF), Dk. Tausi Kida aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Meneja Mradi wa Kampuni Binafsi ya Geowind Power Tanzania na mbunge mstaafu, Victor Mwambalaswa, aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB).

Rais Samia pia amemteua Mkurugenzi Mwanzilishi Mwenza wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Tanzania Data Lab (dLab), Omar Bakari, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITIF).

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya SSC Capital, Salum Hagan, ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) huku Prof. Andrew Temu, Mwenyekiti wa Bodi ya Trustees of the Private Agricultural Sector Support (PASS), akiteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA).

Rais pia amemteua Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) wakati Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa Kampuni ya Nyanza Bottling Co.Ltd ya jijini Mwanza, ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB).

Balozi Mwanaidi Maajar ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Jaji mstaafu Damian Lubuva aliyemaliza muda wake. Rais Samia pia amemteua Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), akiendelea kwa kipindi cha pili.

"SACP Mzee Ramadhan Nyamka, Kaimu Kamishna wa Magereza, Huduma za Urekebu, ameteuliwa kuwa Kamishna Mkuu wa Jeshi la Magereza, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Meja Jenerali Suleiman Mzee aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Uteuzi huo pia umemgusa Venance Mwase ambaye amekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO. Mwase alikuwa anakaimu nafasi hiyo.

# Kamati yaingilia mkataba ujenzi maghala chakula

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imebaini kusuasua kwa mradi wa ujenzi wa maghala ya hifadhi ya chakula na kuagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kukamilisha mazungumzo na mkandarasi anayetekeleza miradi hiyo katika mikoa minane nchini.

Pia NFRA imeagizwa kuhakikisha usalama wa chakula unaendelea kuwapo nchini.

Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea taarifa ya utendaji wa wakala huo.

Alisema NFRA wamekuwa wakitekeleza mradi wa kuongeza uwezo wa uhifadhi wa nafaka kutoka tani 251,000 hadi tani 500,001 na mradi huo ulipata mkopo kutoka serikali ya Poland wa Dola za Marekani milioni 55 na serikali ya Tanzania imechangia Dola za Marekani milioni 12.84.

Alisema kupitia mradi huo, maghala hayo yanajengwa kwenye maeneo mbalimbali katika mikoa minane ambayo ni Manyara, Katavi, Njombe, Songwe, Songea, Dodoma, Rukwa na Shinyanga.

"Walipata hitilafu kidogo na mkandarasi ambapo kamati imeagiza mchakato wa mazungumzo ufike mwisho maana kuna mikataba miwili baina ya serikali ya Poland na Tanzania na mwingine ni mkandarasi na NFRA. Ilipotokea UVIKO-19, mkandarasi alitoa wafanyakazi wake raia wa Poland kwenda kwao.

"Walishindwa kurudi kwa wakati kwa sababu ya mazuio yaliyokuwapo katika nchi mbalimbali na baadaye waliomba kuongezewa muda lakini baada ya hapo, mkandarasi alisema mkataba unaelekea kuwashinda na NFRA walikuwa wanasukuma mradi ukamilike kwa wakati," alisema.

Alisema kutokana na hitilafu hiyo, mazungumzo ya kimkataba yanaendelea kufanyika sambamba na mazungumzo baina ya Tanzania na Poland.

"Kazi yenyewe ilivyoanza ilitakiwa kuanza mwaka 2016, baadaye makandarasi wale waliomba wasiwasilishe hakikisho la malipo ya awali wanavyopewa, baadaye waliingiza mazungumzo baina ya serikali na serikali na moja ya masharti ya ule mkataba ilikuwa makandarasi kutoka Poland washirikiane na makandarasi wazawa wa Tanzania kwa hiyo ilichukua muda hadi kukubaliana," alisema.

Alisema na muda mwingine ulipotea kwenye ugonjwa wa Corona na kusababisha mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CRISPIN FRANCIS OCHANDA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – GOBA | J & J RECOVERIES | 12-09-2022 |
| 2 | HALIMA SOLOMON KHAHOLA | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO – MABWEPANDE | J & J RECOVERIES | 12-09-2022 |
| 3 | BELTOD KULIKIZA KARATWA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – YOMBO VITUKA | J & J RECOVERIES | 12-09-2022 |
| 4 | RAJABU HAMIS BAD | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIMARA STOP OVER | J & J RECOVERIES | 12-09-2022 |
| 5 | DOREEN DANIEL MAJULA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - GOBA | J & J RECOVERIES | 12-09-2022 |
| 6 | ESTHER ABDALAH BHUNGURUMO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TEGETA WAZO | J & J RECOVERIES | 12-09-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

2170154O1

# NSSF yafadhili mfumo taarifa za diaspora

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, zimeingia makubaliano kufadhili matengenezo ya mfumo wa kidigitali wa utunzaji wa taarifa za Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) kwa gharama ya Sh. milioni 50.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana katika ofisi ndogo za wizara hiyo, jijini Dar es Salaam. Ibrahim Maftah, Mkurugenzi wa Uthaminishaji, Takwimu na Usimamizi wa Hadhari alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na Balozi James Bwana, Mkurugenzi wa Idara ya Diaspora katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Joseph Sokoine.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Balozi Bwana aliishukuru Bodi ya Wadhamini ya NSSF na Menejimenti kwa kukubali kufadhili matengenezo ya mfumo huo ambao utakapokamilika utawatambua, kuwasajili na kutunza taarifa za diaspora wa Tanzania waliotapakaa duniani kote na kupata huduma muhimu kutoka kwenye nchi yao.

Balozi Bwana alisema mfumo huo utakuwa chachu ya ushiriki wa diaspora wa kitanzania kidigitali katika shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwamo biashara, uchumi na uwekezaji licha ya umbali waliopo.

"Kwa niaba ya uongozi wa wizara na serikali kwa ujumla natoa shukurani za dhati kwa uongozi mzima wa NSSF wa kukubali kushirikiana nasi katika jambo hili muhimu kwa kutoa Sh. milioni 50," alisema.

Balozi Bwana alisema NSSF ni wadau muhimu wa kutoa huduma kwa diaspora na kwamba pamoja na huduma hizo kupitia dirisha la uwekezaji, wizara imekuwa na mazungumzo na NSSF ili kuangalia namna wanavyoweza kushirikiana zaidi katika eneo la uwekezaji kupitia uendelezaji wa viwanja vilivyopo katika ofisi za ubalozi za Tanzania nje ya nchi.

Alisema mfumo huo pia utawezesha kutekeleza kwa vitendo azma ya serikali kuhamasisha taasisi mbalimbali nchini kuwekeza katika digitali ili kuongeza tija ya matumizi sahihi ya muda wanaohudumiwa na kupunguza urasimu, pamoja na kuiwezesha wizara hiyo kwenda sambamba na dunia katika teknolojia.

Naye Maftah akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema mfuko unatambua na kuthamini mchango wa diaspora katika kujenga uchumi wa taifa.

Maftah alisema ushiriki wa NSSF katika kufanikisha kuanzishwa kwa mfumo huo unatokana na umuhimu wa suala lenyewe, lakini kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha diaspora wanachangia kikamilifu maendeleo ya uchumi wa taifa.

"Wakati wote NSSF imekuwa mmoja wa wadau muhimu katika shughuli na matukio mbalimbali ya diaspora, hivyo kupitia mfumo huo ni fursa kwa mfuko kutangaza fursa mbalimbali za miradi ya uwekezaji kama vile nyumba, viwanja, hoteli na huduma nyingine zinazotolewa na NSSF," alisema.

Aliipongeza wizara kwa kubuni wazo hilo la kuanzisha mfumo huo ambao utakuwa chachu ya mafanikio mbalimbali ya kuwaunganisha Watanzania waliopo nje ya nchi na fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Mwakilishi wa Kitengo cha Diaspora Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Semeni Nandonde, alisema kupitia mfumo huo, serikali itafahamu idadi ya diaspora, ujuzi walionao, elimu pamoja na kupata huduma maalum ambazo zitaandaliwa kwa ajili yao kama vile huduma za hifadhi ya jamii, benki, bima ya afya, uwekezaji, biashara na masoko.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akikabidhi zawadi ya ngalawa kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Hossein Amir Abdollahian, baada ya mazungumzo yao na ujumbe wake Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# TRA yatoa ufafanuzi utozaji kodi ya pango

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imesema kodi ya pango siyo mpya, bali wigo umeongezwa kwa wapangishaji wa nyumba binafsi kama ilivyokuwa kwa wenye nyumba za biashara.

Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi ilitoa ufafanuzi huo jana kupitia taarifa yake iliyoitoa kwa vyombo vya habari ikisisitiza kuwa kodi hiyo siyo mpya.

"Tunapenda kuwafahamisha wananchi kuwa kodi hii siyo mpya, bali wigo umeongezwa ili wapangishaji wa nyumba binafsi wenye pato linaloanzia Sh. 500,000 kwa mwaka na kuendelea, wajumuishwe kwenye wigo wa kodi kuanzia Julai Mosi 2022," ilisema taarifa yao.

Idara hiyo pia ilisema mwenye nyumba atapata cheti cha kodi ya zuio kama ushahidi wa malipo ya kodi iliyolipwa kutokana na zuio la asilimia 10.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo, alisema kodi hiyo hailipwi na mpangaji, bali anakatwa kwenye kodi ambayo anatakiwa kumlipa mwenye nyumba.

"Hii siyo kodi mpya isipokuwa kuna wale walikuwa wapangishaji binafsi ambao wapo chini ya Sh. 500,000 na walikuwa hawalipi kodi ya pango, kilichofanyika ni kuwajumuisha pia, mwanzoni ilikuwa ni Sh. 500,000 kuendelea na zile nyumba za biashara ndizo zilikuwa zinatozwa.

"Mpangaji ndiyo alikuwa anakata, anazuia hii asilimia 10 kwa sababu inafanyika hivyo kwa sababu anayepanga ndiye anayeshikilia kipato cha mwenye nyumba, ndiyo maana wakati wa kulipa tunataka azuie asilimia 10 aiwasilishe TRA," alifafanua.

Alisema uamuzi huo unaongeza wigo wa kodi kwa sababu wanaopangisha nyumba kwa Sh. 500,000 kushuka chini ni wengi.

## Msako vifungashio plastiki nchi nzima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ametangaza kuanza kwa operesheni kabambe ya kutokomeza vifungashio vya plastiki ambavyo vimegeuka kuwa vibebeo Agosti 29, mwaka huu kwenye mikoa yote nchini.

Operesheni hiyo itaguswa maeneo yote ikiwamo masoko, maduka, magulio pamoja na bucha za nyama na samaki.

Vilevile, Dk. Jafo ametoa miezi miwili kwa watendaji wake kupitia upya kanuni ili kubana vifungashio hivyo kugeuka kuwa vibebeo.

Dk. Jafo, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipozungumza na wataalamu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), waliokutana kujadili utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

Alisema, hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyeagiza mikoa yote nchini kuhakikisha wanapambana na matumizi ya mifuko ya plastiki.

"Operesheni hii itakuwa endelevu na usimamizi wa katazo la mifuko ya plastiki na masuala mengine ya kimazingira, kwa hiyo itakuwa ni moja ya majukumu ya kawaida ya usimamizi wa mazingira kwa ngazi za wilaya kupitia vyombo vya usalama ngazi za wilaya pamoja na maofisa mazingira wa ndani ya halmashauri kwa kushirikiana NEMC," alisema.

Alisema, kanuni ya sita ya mwaka 2019 ya kutokomeza mifuko ya plastiki ilipiga marufuku mifuko hiyo lakini iliruhusu vifungashio kwa lengo kubwa kwamba kuna baadhi ya bidhaa lakini kuna watu wasio waaminifu wamegeuza vifungashio kuwa vibebeo.

Aliwataka kwenye operesheni hiyo wakuu wa mikoa na wilaya wahakikishe wanashirikiana na viongozi wa masoko na magulio ili kuhakikisha mazingira yanakuwa salama.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema kamati za ulinzi na usalama kwenye wilaya na mikoa zinatakiwa kusaidia suala hilo ili kupata mafanikio ya operesheni hiyo.

"Kuna tatizo la uaminifu kwenye viwanda vilivyopewa leseni ya kuzalisha mifuko, tumeenda Tabora tumekuta wauzaji wana vifungashio vya aina mbili ambavyo vya kwanza ni vinavyokubalika vina viwango sawa kulingana na matakwa ya TBS, vingine havina viwango, walipoulizwa walisema walinunua mzigo ambao haukuwa na shida lakini walipofungua walikuta aina mbili za mifuko," alisema.

Pia, alisema kutokana na kubainika kuwa NEMC inafanya msako kwenye masoko sasa vifungashio hivyo vimepelekwa kwenye magulio na kuomba TAMISEMI kusaidia kwenye eneo hilo.

## TEA yatekeleza miradi 3,314 toka kuanzishwa

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Elimu (TEA) imesema tangu kuanzishwa kwake, imetekeleza miradi 3,314 yenye thamani ya shilingi bilioni 212.6.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Bahati Geuzye, wakati akizungumzia majukumu ya taasisi hiyo hivi karibuni na utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Alisema taasisi za elimu zikiwamo shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu vimenufaika kwenye miradi mbalimbali.

Gauzye alisema kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, ukarabati mkubwa wa miundombinu ya elimu ulifanyika na TEA imeratibu ukarabati wa shule kongwe 17 za sekondari kati ya 89 zilizoko kwenye mpango wa ukarabati.

Alizitaja shule hizo kuwa ni Ngaza, Ilboru, Same, Msalato, Mzumbe, Mwenge, Tabora Wasichana, Tabora Wavulana, Kilakala, Pugu, Sengerema, Ruvu, Korogwe Wasichana, Dodoma, Bihawana, Kondoa na Bwiru Wasichana.

Pia alisema Mfuko wa Elimu tangu kuanzishwa kwake umetoa ufadhili wa miradi ya elimu katika vyuo vya elimu ya juu na miradi iliyofadhiliwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa kumbi za mihadhara.

Alitaja mambo mengine kuwa ni ujenzi wa mabweni, ununuzi wa vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), maabara na vifaa vingine vya kujifunzia na kufundishia katika vyuo 11 vya elimu ya juu.

Mamlaka, alisema imetekeleza programu ya kuwezesha wanafunzi wa kike kujiunga na kozi za sayansi na teknolojia katika vyuo vikuu na vya kati ambapo wanafunzi 594 walinufaika na programu hii kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mkurugenzi huyo alisema kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaoratibiwa na TEA, katika mwaka wa fedha 2021/22, Sh. bilioni 8.6 ziligharamia ufadhili wa miradi 160 ya kuboresha miundombinu ya elimu katika shule 151 nchini.

Alisema Mfuko wa Elimu unapata fedha kutokana na vyanzo vya kisheria vilivyoainishwa katika Sheria ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya mwaka 2001.

Alitaja vyanzo hivyo kuwa ni pamoja na fedha zinazotoka kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kwamba mfuko pia unapokea michango ya fedha na vifaa kutoka kwa wadau wa elimu.

Aliishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Mfuko wa Elimu na Mfuko wa Kuendeleza ujuzi.

# Wanafunzi 600 wa kike kunufaika ufadhili wa Rais Samia vyuo vikuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ametangaza nafasi 600 kwa wahitimu wa kidato cha sita waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi, kuomba mikopo ya elimu ya juu kupitia ufadhili wa Rais Samia (Samia Scholarship) ili kujiendeleza kitaaluma.

Pia amewataka wananchi kuendelea kutoa maoni kwa njia ya mtandao ya kuboresha rasimu ya sera ya sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kabla ya kuanza kufanyiwa kazi na serikali.

Mkenda alibainisha hayo alipokuwa akifunga mkutano wa wadau mbalimbali wa kujadili na kutoa maoni ya rasimu hiyo jana jijini hapo.

Alisema nafasi hizo ni kwa ajili ya kusoma katika vyuo vya elimu nchini ili kujiendeleza katika taaluma ya mchepuo wa masomo ya sayansi.

"Naomba wanafunzi waliofaulu masomo ya sayansi waombe mikopo kupitia ufadhili huo. Nafasi zilizopo ni nyingi, hivyo wanapaswa kutumia fursa hiyo kuomba mikopo ya elimu ya juu," alisema Prof. Mkenda.

Waziri alisema lengo la kutoa ufadhili huo ni kuona wanafunzi wanaweka jitihada katika masomo ya sayansi ili kupata watafiti wa kutosha baadaye.

Kadhalika, aliwataka wananchi kuendelea kutoa maoni yao kwa njia ya mtandao kabla ya shughuli ya kukusanya maoni kufungwa.

Alisema maoni yaliyotolewa katika mkutano huo serikali itayazingatia ikiwamo kuyafanyia kazi ili kuiboresha rasimu hiyo ambayo ni muhimu kwa jamii na taifa.

"Tunazaidi ya maoni lakimoja katika mitandao tunaomba waendelee kuyatoa ili kuzidi kuboresha sekta hiyo," alisema Prof. Mkenda.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, alisema kikao hicho kimekuwa na matokeo chanya, kutokana na wadau kutoa maoni yao kwa wingi.

Dk. Nungu alisema anaamini maoni yao yatafanyiwa kazi huku akisisitiza waende wakawe mabalozi wazuri katika maeneo wanayotoka.

Naye Mkurugenzi wa Sayansi Teknolojia na Ubunifu, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema serikali imeweka jitihada katika kuhakikisha wanasimamia sekta hiyo ili izidi kuimarisha.

Prof. Kipanyula alisema sekta ya ubunifu ni muhimu sana hivyo kila mmoja azingatie maoni aliyotoa ikiwamo kuelimisha jamii ili kuendelea kutoa maoni katika mtandao.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akisalimiana na Spika wa Bunge la Zambia, Nally Mutti, katika Mkutano wa 65 wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA), katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Halifax, Nova Scotia, nchini Canada jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# GCLA yawafunda madereva kemikali

**Na Mary Geofey**

MADEREVA wanaosafirisha kemikali hatarishi wametakiwa kupata elimu ya usimamizi na usafirishaji salama wa kemikali hatarishi na kufuata kanuni na sheria za usafirishaji wa kemikali nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, David Elias, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofunga mafunzo ya siku mbili ya madereva 140 wanaosafirisha mizigo ya kemikali yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kupitia Ofisi ya Kanda ya Mashariki.

"Wasafirishaji wote wa kemikali hatarishi mnatakiwa kisheria kuwa na vibali vyote ambavyo vinahitajika wakati wa kusafirisha kemikali na kuhakikisha kemikali zinasafirishwa kwa usalama na dereva awe amepitia mafunzo ya usafirishaji salama wa kemikali ili kuondokana na athari pale inapotokea majanga wakati wa usafirishaji wa kemikali," alisema Elias.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa mafunzo ya usafirishaji salama wa kemikali yatolewe kwa wamiliki wa magari na kampuni kwa lengo la kuwajengea uelewa juu ya faida ya kuwapeleka madereva na wasimamizi wa kemikali kupata elimu hiyo na kuelewa shida zinazowakabili madereva pindi wanaposafirisha kemikali na namna ya kuzitatua.

Pia aliwasisitiza madereva kuzingatia kanuni na sheria za usafirishaji wa kemikali hatarishi ili kuepusha kuleta madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo, aliwataka madereva kufahamu na kutambua aina za kemikali wanazosafirisha ili kuchukua tahadhari kabla na wakati wa kusafirisha kemikali kwa kuwa usafirishaji wa kemikali unahitaji umakini mkubwa.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Ali Mhina, dereva kutoka Kampuni ya Tazama Pipe Line, alipongeza GCLA kwa kutoa mafunzo kwa madereva kwa kuwa kunamjenga dereva kujitambua, kuwa makini na kuitambua jamii.

"Tunaipongeza mamlaka na Wizara ya Afya kwa kutambua umuhimu wa afya na usalama wa dereva na kuhakikisha dereva anasafirisha kemikali kwa usalama.

"Mafunzo haya yatatusaidia katika kusafirisha mizigo ya kemikali kwa usalama mkubwa kulinganisha na tulivyokuwa tunaifanya kazi hii kabla ya mafunzo haya," alipongeza Ali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sputanza lisimamieni hili kwa umakini mkubwa sana

**CHAMA** cha Wachezaji Soka Tanzania (Sputanza), kimepinga hatua za baadhi ya klabu zinazotaka kuwatoa wachezaji wake kwa mkopo bila wao kukubali.

Mwenyekiti wa chama hicho, Mussa Kisoki, amenukuliwa akisema, ili klabu imtoe mchezaji kwa mkopo kwenda kwenye klabu nyingine ni lazima mwenyewe aridhie na kitendo cha kumlazimisha ni kosa, ambapo sisi pia tunaunga mkono.

Kauli ya Kisoki, imekuja baada ya kuripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa klabu mbalimbali zinatarajia kuwatoa wachezaji wao kwa mkopo kwenda kwenye klabu zingine ikiwa ni siku chache tu kabla ya dirisha kubwa la usajili kufungwa.

Kwa mujibu wa Kisoki, mchezaji ana haki ya kuhoji anakopelekwa, kule anakokwenda ni lazima ajue anaenda kuongeza kipaji chake au kuua, au anakwenda kuongeza kipato chake, au kitapungua.

Na kwamba, asiporidhia ni lazima abaki na timu yake, au uvunje mkataba kwa kumlipa mshahara wake wote wa muda waliomsajili na fedha yake ya usajili.

Katika hili, Nipashe tunaiunga mkono Sputanza kwa asilimia 100, kwa sababu mtindo huu ukiendelea kuchekewa athari zake ni kubwa sana kwa wachezaji wetu kwa siku za usoni.

Timu kubwa hasa Simba na Yanga zimekuwa na tabia ya kumtaka kila mchezaji wanayemwona mbele yao, matokeo yake hujikuta wamefanya usajili wa wachezaji ambao hawakuwa wakiwahitaji au kujaza wachezaji wengi kwenye nafasi moja.

Kwa maneno mengine timu hizi kubwa zinapenda kufanya usajili wa kukomoana kwa kuwahi kila mchezaji ambaye anaonekana kuwa na kiwango cha juu, hata kama hawana mahitaji nae.

Matokeo yake mfumo wa kocha unakuwa tofauti na wachezaji aliowakuta na hivyo kulazimika wengine kuwakataa na pale timu inaposhindwa pakuwapeleka, hulazimika kuingia makubaliano ya kuwatoa kwa mkopo.

Tofauti ya mikopo iliyozoeleka kwa ligi zilizoendelea na hii yetu ni kwamba, kwanza mchezaji analazimishwa kuondoka, pili analazimishwa kukubali kupunguziwa mshahara wake kama atataka kubakia na timu husika. Kiukweli hiyo siyo haki hata kidogo, kwa sababu kila mchezaji ndoto zake ni kukuza kipaji chake ili afikie kiwango cha juu kabisa na ikiwezekana hata kupata timu nje ya nchi.

Ikumbukwe kwamba, soka ndio ajira yake na ina ukomo wa umri, mchezaji hupendelea kwenda kujiunga na timu kubwa ili aweze kuongeza kipato chake kwa upande wa mshahara na marupurupu mengine.

Hivyo, suala la kumlazimisha mchezaji kuondoka au kupunguziwa mshahara wake maana yake unamnyima haki yake kimsingi na kumrudisha nyuma kabisa katika ndoto zake alizojiwekea.

Taarifa za hivi karibuni zinaonesha kuwa kunaweza kukawa na kesi nyingi baada ya dirisha la usajili kufungwa Agosti 31, mwaka huu.


Kwani, taarifa zinasema kuna wachezaji wengi wamegoma kuondoka kwenye klabu walizosajiliwa, kwa sababu kule wanakotaka kupelekwa hawaoni kama kunaweza kuwaimarisha kisoka.

Nipashe, tukiwa kama wadau wakuu wa mchezo wa soka, tunazishauri klabu kukaa na kuzungumza na kufikia makubaliano na mchezaji husika kama wanataka kumtoa kwa mkopo.

Pia, wachezaji wenyewe wanatakiwa kuwa makini na mikataba ambayo wanaingia na timu hizo na pia kutokukubali kirahisi kuhamishwa timu au kukatwa mishahara yao. Kubwa wanaloweza kufanya ni kufikia makubaliano ya kuvunjwa kwa mkataba walioingia ili waweze kulipwa stahiki zao zote na kuendelea kutafuta maisha na kukuza vipaji vyao vya uchezaji katika timu nyingine.

Nalo shirikisho la soka Tanzania, TFF, ambalo ndio mlezi na msimamizi mkuu wa timu zote, linatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kulisemea hilo, ili kama mchezaji na klabu wanataka kuachana, basi waachane kwa utaribu ulionyooka na wenye maslahi kwa pande zote mbili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kila la heri Simba Queens Ligi ya Mabingwa

**KWA** mara ya kwanza kwenye historia ya soka nchini, timu kutoka Tanzania Simba Queens inacheza fainali ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati kwa soka la wanawake, CECAFA, ikisaka tiketi pia ya kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Timu hiyo imefanikiwa kuingia fainali na kuweka rekodi ya timu ya wanawake kutoka Tanzania kucheza fainali hizo kwa mara ya kwanza baada ya kuchabanga AS Kigali mabao 2-1 kutoka nchini Rwanda, Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Leo hii inacheza fainali na She Corporate ya Uganda kwenye Uwanja wa Chamazi, Dar es Salaam.

Bingwa wa michuano hiyo, atauwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye fainali za Ligi ya Mabingwa zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Iwapo Simba Queens itashinda basi itaweka historia ya kuwa timu ya kwanza kwa wanawake Tanzania upande wa soka kuiwakilisha nchi kwenye fainali hizo.

Simba Queens haitaiwakilisha Tanzania tu, bali ukanda wote wa Afrika Mashariki. Kwanza kabisa napenda kuipongeza timu hiyo kwa hatua ambayo wamefikia.

Ukikiangalia kikosi hicho tangu kilipoanza michuano hiyo unakiona kuwa si tu kama kina wachezaji wenye uwezo mkubwa, lakini wanajituma na njaa ya mafanikio.

Wanapocheza wachezaji wa Simba Queens unaona kabisa jinsi wanavyojituma kupambania jezi au nembo ya klabu yao.

Nilisikia hata baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba wakisema kuwa kama timu ya wanaume ingekuwa inacheza kama vile, basi kwa uwezo ilionao wasingefungwa na timu yoyote.

Wanasimba wenyewe wanaamini kuwa wana kikosi kizuri cha wachezaji, lakini tatizo ni kwamba hawajitumi kama ilivyo kwa timu ya wanawake.

Nirudie tena kwa kinadada ni kwamba baada ya kuishia nusu fainali msimu uliopita nchini Kenya, inaonekana viongozi walifanya tathmini ya kutosha na kugundua mapungufu kadhaa ambayo yamefanyiwa kazi.

Ni kwamba wamesajili wachezaji kadhaa kutoka nje ya nchi ambao wamekuja kuitoa pale ilipoishia na kuipeleka mbele.

Usajili wa kina Olaiya Barakat kutoka Nigeria, Vivian Aquino kutoka Kenya, Daniela Ngoi, beki wa kati ambao msimu uliopita aliichezea Yanga Princess raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Pambani Kuzoya ambaye ni raia wa Congo DR, kumeifanya timu hiyo kuimarika zaidi na kuifanya kuwa tishio.

Kuna wataalamu waliwaambia viongozi na benchi la ufundi Simba kuwa wana wachezaji wazuri, lakini inabidi watafute baadhi ya wachezaji wenye miili mikubwa hasa kwenye maeneo ya kiungo wa kukaba na mabeki wa kati. Na hilo limefanyika kwa kiwango kikubwa. Uwekezaji uliofanywa kwa uongozi wa Simba unaonyesha kabisa kuwa unataka kufanya mapinduzi makubwa ya soka kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa upande wa wanawake.

Wakati wamepambana na kuifanya timu ya wanaume ya Simba kuwa moja kati ya timu kubwa na zinazoogopeka kwa sasa barani Afrika hasa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, sasa taratibu inaonekana wanaishika mkono timu ya wanawake nayo kuifanya kuwa tishio Afrika kwa upande wa wanawake. Na nionavyo ni kwamba upande huu wa kinamama inaweza kupata mafanikio makubwa kwa muda mfupi kuliko hata timu ya wanaume. Iwapo Simba itashinda kwenye mechi ya leo na kwenda fainali, ikifanya marekebisho madogo tu upande wa golikipa, inaweza kufanya makubwa, kwani inaweza kuwa timu ya kwanza kuingia nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa kabla ya timu ya wanaume haijafanya hivyo.

Huu ni mfano wa kuigwa na klabu zingine nchini kuwekeza kwenye soka la kinamama kwani taratibu linaonekana kuanza kukua, na kujipatia mashabiki.

Tumeona jinsi wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walivyojitokea kwa wingi kwenye mechi zao kama vile wanavyoenda kuishangilia timu ya wanaume.

Nina wasiwasi klabu zingine zikishtuka na kuona soka hilo limekuwa na mashabiki wengi na kuanza kuwekeza, tayari Simba Queens itakuwa ipo mbali sana. Fainali ni fainali tu, chochote kinaweza kutokea, lakini kwa jinsi nilivyoiona Simba Queens tangu mwanzo, inaonekana ni timu bora zaidi kuliko zote msimu huu. Imecheza mechi nne ikishinda zote, imefunga mabao 17 na kufungwa bao 1-0.

Hata timu inayocheza nayo She Corporate ya Uganda imeshacheza nayo kwenye hatua ya makundi, zote zikiwa Kundi B, lakini Simba ilishinda mabao 2-0.

Na nilivyoishuhudia mechi hiyo ni kwamba, Simba Queens ilikosa mabao mengi sana, kama ingekuwa makini, basi ingeibebesha mzigo wa mabao. Pamoja na kwamba huwezi kutabiri fainali, lakini naipa nafasi kubwa Simba Queens ambayo pia inaonekana ina kikosi kizuri pia cha kwenda kupambana kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Taasisi yaandaa maonyesho biashara kumpongeza Samia

**Na Halfani Chusi**

TAASISI ya Mamaz and Papa's Community Reform, yenye makao yake makuu Mkuranga mkoani Pwani, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imeandaa maonyesho ya kimataifa ya biashara yatakayotarajiwa kufanyika Oktoba 14 hadi 23, mwaka huu.

Maonyesho hayo yatakayojulikana kama 'Mama Samia International Mkuranga Exhibition', yamelenga mambo mbalimbali ikiwamo kuunga mkono juhudi za serikali ya Rais Samia katika kukuza uchumi wa nchi.

Taarifa iliyotolewa jana na Mratibu wa Taasisi hiyo, Omary Kombe, ilisema mbali na kuunga mkono juhudi za Rais, maonyesho hayo yatasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na kuongeza pato la taifa.

"Maonyesho haya yana lengo la kutoa fursa kwa wawekezaji, wafanyabiashara wenye viwanda, sekta ya utalii na wajasiriamali wadogo kuuza biashara zao na kujitangaza kitaifa na kimataifa pamoja kuutangaza mkoa wa Pwani na taifa kwa kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara," alisema Kombe.

Alisema kufanikisha maonyesho hayo yatakayokuwa na kaulimbiu 'Tuko Tayari kwa Uwekezaji wa Viwanda, Biashara, Kilimo na Utalii Kazi Iendelee', kiongozi huyo aliwaomba wadau wa maendeleo kujitokeza kudhamini maonyesho hayo ili kuunga mkono juhudi hizo.

"Naomba wadau wa maendeleo tujitokeze kudhamini maonyesho haya lakini ada kwa washiriki ni ndogo sana kulinganisha na maonyesho mengine. Mfano wawekezaji kutoka nje ya nchi watalipa Dola 500 za Kimarekani na wawekezaji wa ndani watatoa Sh. 500,000 kwa siku zote za maonyesho.

"Kwa wale wajasiriamali wa kati watalipia Sh. 100,000 na wale wadogo watalipia kuanzia Sh. 20,000 kwa hiyo fomu zitasambazwa kuanzia Septemba Mosi katika vyombo mbalimbali na maeneo maarufu hapa nchini," alisema.

Maonyesho hayo tayari yameshapata kibali cha kufanyika kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Maendeleo ya Biashara.




Mkaguzi wa magari kutoka Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Kahama, Josia Sakala, akikagua mifumo ya breki kwenye moja kati ya magari 60 ya shule za msingi za binafsi, wilayani humo, mkoani Shinyanga jana, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Kamanda wa Polisi wa Kikosi hicho, Wilbrod Mutafungwa, kuhakikisha magari yote ya kubeba wanafunzi yanakaguliwa ili kuzuia ajali. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Magari 50 yazuiwa kusafirisha wanafunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAGARI 50 yanayobeba wanafunzi wa shule zinazomilikiwa na watu binafsi Kahama mkoani Shinyanga, yameondolewa namba za usajili na kuzuiwa kufanya kazi baada ya kubainika kuwa mabovu.

Hatua hiyo imechukuliwa ili kunusuru wanafunzi kupata ajali wanapokuwa barabarani kwenda na kutoka shuleni.

Magari hayo yamebainika kuwa na dosari ya mifumo ya breki, viti na mikanda, sakafu kutoboka na kuingiza vumbi, usukani na kutokuwa na viakisi mwanga.

Kutokana na hatua hiyo, magari yamepigwa marufuku kuingia barabarani mpaka yatakaporekebishwa kasoro hizo na wamiliki.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Kahama, Flora Nangawe, aliyabainisha hayo jana wakati wa utekelezaji wa agizo la Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbrod Mutafungwa. Mutafungwa aliagiza magari yote ya kubeba wanafunzi yakaguliwe ili kuzuia ajali.

Alisema magari 60 yalikaguliwa na kati ya hayo, 50 yalibainika kuwa na dosari na kuondolewa namba za usajili huku yakizuiwa kubeba wanafunzi mpaka yatakaporekebishwa na manane yakihitaji maboresho madogo na mawili yalioneka na mazima yanayofaa kuendelea kubeba wanafunzi.

Pia alisema hakuna gari lolote litakaloruhusiwa kubeba wanafunzi kama halijarekebeshwa dosari zilizobainika wakati wa ukaguzi kwa kuwa siku ya kufungua shule kutakuwa na ukaguzi wa magari hayo na ikibainika liliondolewa namba za usajili na limebeba wanafunzi mmiliki wake atawajibika kisheria.

"Magari yote yaliyobainika kuwa na dosari ya mifumo ya breki, sakafu kutoboka, matairi kuisha wahakikishe wanayarekebisha kabla ya siku ya kufungua shule Septemba 5, mwaka huu na shule zinapofunguliwa hakuna gari lolote litakaloruhusiwa kubeba wanafunzi, hivyo siku hiyo wamiliki wote wa shule tusije kulaumiana," alisema Nangawe.

Mmiliki wa Shule ya Green Star, Davidi Ndugi, alisema ubovu wa magari unasababishwa na kuwapo miundombinu mibovu ya barabara iliyoko katika Manispaa ya Kahama.

## Msanii mbaroni tuhuma za kutengeneza silaha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamshikilia msanii mwanaume (32) kwa tuhuma za kukutwa na silaha bandia za kivita.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, aliwaambia waandishi wa habari jana ofisini kwake Kibaha kuwa mtuhumiwa huyo (jina linahifadhiwa) alikamatwa Agosti 25, mwaka huu, majira ya saa 10 jioni huko Sanze, Kata ya Kisarawe.

Kamanda Lutumo alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kukutwa na silaha aina ya AK 47 (SMG) 11, Uzgun moja, bastola tano, mavazi ya kukinga risasi mawili yaliyotengenezwa kwa risasi na mbao pamoja na radio call bandia moja.

Katika mahojiano yao na mtuhumiwa, Kamanda Lutumo alidai alikiri kutengeneza mwenyewe silaha hizo ili atumie kwa matumizi yake.

Kamanda Lutumo alisema upelelezi kuhusiana na tukio hilo unaendelea na ukikamilika, atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Kufuatia tukio hilo, Kamanda Lutumo alitoa wito kwa wananchi kufuata sheria na kama wanahitaji kutumia silaha, wafuate taratibu za kupata vibali kutoka taasisi husika.

Alisema uzoefu unaonyesha kuwa yapo matukio ya watu wanatishiwa na silaha zinapofuatiliwa inabainika kuwa ni bandia.

**Kamanda Lutumo alisema upelelezi kuhusiana na tukio hilo unaendelea na ukikamilika, atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.**

# Tril. 1.15/- kujenga shule mpya na kumaliza uhaba wa miundombinu

**Na Neema Hussein,** KATAVI

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. trilioni 1.15 kwa ajili ya kujenga shule mpya za msingi kwenye maeneo ambayo hayana shule na kuongeza miundombinu kwenye shule ambazo zina upungufu wa miundombinu.

Sehemu ya fedha hizo pia itatumika kufanya ukarabati kwenye shule kongwe ambazo miundombinu imechakaa ili kuondoa matatizo katika sekta ya elimu ndani ya miaka mitano. Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema hayo juzi baada ya kupokea taarifa fupi kuhusu maendeleo ya elimu ndani ya mkoa wa Katavi huku akisema mkoa una wajibu wa kujua zaidi ya wanafunzi 1,000 ambao hawajaripoti kidato cha kwanza wako wapi na wanafanya nini. Kipanga alisema ndani ya miaka hiyo, pia wanaondoa changamoto ya kukosekana kwa shule za sekondari katika maeneo ambayo hayana shule kwa kujenga shule 1,026 zikiwamo 1,000 katika ngazi ya kata na 26 katika ngazi ya mikoa ambazo ni za wasichana.

"Niwatoe hofu kutokana na changamoto hizi mlizozisema hapa za upungufu wa madarasa, madawati, meza, matundu ya vyoo na nyumba za walimu pamoja na miundombinu mingine, tunakokwenda sasa ni kuzuri na dhamira ya Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) sasa inaanza kujifafanua," alisema Kipanga.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema wamepokea walimu wapya 291 ndani ya mkoa ambao watasaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kuufanya mkoa uendelee kufanya vizuri katika elimu.

Akisoma taarifa mbele ya Naibu Waziri, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Katavi, Elpidius Baganda, alisema changamoto zinazoikabili sekta ya elimu katika mkoa ni pamoja na upungufu wa vyumba vya madarasa, meza, viti na matundu ya vyoo.

Naibu Waziri Kipanga yuko mkoa wa Katavi kwa ziara ya siku mbili kuangalia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika sekta ya elimu.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Shoughle (katikati), akishirikiana na waombolezaji kubeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa katibu wa babalishe katika soko la Feri, jijini Dar es Salaam, Yusuf Boli, aliyezikwa katika makaburi ya Mbagala Kipati wiki hii.. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Madiwani wataka fedha zilizobaki kuelekezwa miradi ya maendeleo

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu Kahama mkoani Shinyanga, wametaka fedha za bakaa zaidi ya Sh. millioni 805.5 zilizotolewa na halmashauri hiyo zitumike katika utekelezaji wa miradi ambayo haijakamilika.

Agizo hilo walilitoa juzi kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne ya mwaka wa fedha wa 2021/22.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Maganga, alitoa hoja hiyo baada ya Ofisa Mipango wa Halmashauri, Theresia Nsumba, kutoa taarifa ya mpango wa fedha.

Maganga alisema inasikitisha fedha kubaki huku miradi mingi ikihitaji kukamilishwa, hivyo akashauri baada ya mfumo kufunguka, zielekezwe kwenye miradi.

Diwani wa Viti Maalum, Esther Matone, alisema walipitisha miradi ya ujenzi wa stendi kwenye kata za Ulewe Sh. milioni nane, Ubagwe Shilingi milioni tisa na Nyamilanagno lakini hawajaona utekelezaji wake.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu, Lala Gaga, alisema kutokana na ufinyu wa bajeti wataanza kutekeleza mradi wa ujenzi kwa stendi moja kwenye kata ya Nyamilangano na ushauri kuhusu bakaa zitumike kutekeleza miradi wameupokea.

Nsumba alisema kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 walikuwa na bakaa ya Sh. bilioni 1.8 na mwaka 2021/2022 walikuwa na bakaa Sh. milioni 805.5 ikiwa fedha hizo pia zinatumika kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Linno Mwageni, alisema fedha hizo zimeletwa mwishoni mwa mwaka wa fedha na kushindwa kuzifanyia kazi sababu ya mifumo ya utoaji fedha kufungwa.

"Huo ni utaratibu wa kawaida lakini sasa imefunguka na fedha hizo zitachukuliwa kutekeleza miradi mbalimbali iliyokuwa imelala," alisema Mwageni.

# TFS yaanza kumtua mama ndoo kichwani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umeanza kumtua mama ndoo kichwani kwa vitendo kwa kujenga mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 22 katika kijiji cha Butengo, Chato mkoani Geita.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema hayo juzi alipokuwa katika hafla fupi ya uzinduzi wa mradi huo katika kijiji cha Butengo.

"Mwaka huu kaulimbiu ni kumtua mama ndoo kichwani, hivyo TFS tumeanza kuwatua kinamama ndoo kichwani na tunawatua kwa sababu wamekuwa na mchango mzuri kwenye hifadhi hii," alisema.

Masanja aliwataka viongozi wa kata na vijiji kusimamia vizuri mradi huo ili ulete manufaa yaliyokusudiwa ya kutatua tatizo la upatikanaji wa maji.

"Serikali za vijiji, kata muwe makini katika kusimamia mradi huu kwa kuwa hii ni rasilimali yenu na mkiiharibu ni nyie wenyewe. Lakini tunatamani muitunze ili tunapoleta miradi mingine tuone faida za miradi hiyo," aliongeza.

Aidha, amewapongeza wananchi wa Butengo kwa jitihada kubwa wanazozifanya za kulinda Shamba la Miti Silayo, kwa kutunza maeneo ya hifadhi na kuwa na uhusiano mzuri na wahifadhi.

Masanja alitoa rai kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi nchi nzima kuiga mfano wa wananchi wa Butengo ambao kwa hiari yao wamekubali kushirikiana na wahifadhi.

Mbunge wa Chato, Dk. Merdad Kalemani, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupeleka miradi 11 ya maji katika jimbo hilo ukiwamo uliofadhiliwa na TFS. Alisema uwapo wa mradi huo utapunguza tatizo la upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Butengo.

Naye Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Silayo, Juma Mwita, alisema mradi huo uliogharimu Sh. milioni 22.1, unahudumia vitongoji vya Butengo Senta, Butengo na Mwenge na kunufaisha kaya 180 sawa na wastani wa watu 1,080.

Mradi huo, alisema umekuwa msaada mkubwa kwa jamii kwa kuongeza tija katika shughuli za uzalishaji kwani muda mwingi ulikuwa ukitumika kutafuta maji na umewezesha upatikanaji wa majisafi na salama.

Pia alisema mradi huo ambao ulianza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2001/22, umesaidia kupunguza kwa magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama kama kichocho, kuhara na kipindupindu.



# WFP yatoa ndege kukabiliana na maafa

**Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), limetoa msaada wa ndege zisizo na rubani (drones) zenye thamani ya Sh. milioni 102.7 kwa ajili ya kukabiliana na maafa mbalimbali.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alipokea vifaa hivyo jana jijini hapo.

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Naibu Waziri alisema vifaa hivyo vitasaidia Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza shughuli za uratibu na udhibiti wa maafa hasa katika kuchukua taarifa za picha ili kupata majanga na madhara kwa uzuri na kwamba ofisi hiyo inatambua umuhimu wa vifaa hivyo.

"Kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaishukuru sana WFP, kwa kutupatia vifaa hivi muhimu kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano kwa njia ya mtandao na kufanya operesheni za utafutaji na uokoaji, kupata ramani za hatari zilizopo, uwezekano wa kuathiriwa na janga na uwezo wa jamii husika," alisema Nderiananga.

Pia, aliishukuru serikali kwa kuendelea kushirikiana na mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa ambayo yamekuwa yakiunga mkono jitihada zinazofanywa katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi na taifa.

Awali, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dk. John Jingu, alisema ofisi hyo iko tayari kushirikiana na WFP, kwa kila eneo ambalo watahitaji ushirikiano huku akiahidi vifaa hivyo kutumika kama ilivyokusudiwa. "Tunakumbana na maafa mengi na huwa inachukuwa muda mrefu kwa waokozi au upataji wa taarifa unachelewa hivyo, kwa ajili ya hizi drone naamini ufanyaji kazi na upatikanaji wa uhalisia wa tukio utapatikana kwa urahisi," alisema Dk. Jingu.

Alisema, serikali iko pamoja na shirika hilo ili kuhakikisha kila mipango inakwenda sawa kwenye utekelezaji.

Mkurugenzi Mkazi wa WFP, Sarah Gibson, alifafanua kuwa mradi huo ni endelevu kwa miaka mitano kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2027 na shirika litafanya kazi zake kulingana na vipaumbele vya serikali na kuwekeza katika kilimo, elimu, maafa pamoja na wakimbizi.




Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa (katikati), akikabidhi funguo ya Bajaj kwa Mariam Malumbo, baada ya kuibuka mshindi wa promosheni ya Vodacom M-Pesa Imeitika, jijini Tanga jana. Kulia ni Meneja Mauzo Mwandamizi Vodacom Kanda ya Kaskazini, Stratton Mchau. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# Atoweka nyumbani kwa hali ya kutatanisha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MWENGE Samatwa (pichani) mkazi wa Kikuyu Kusini jijini Dodoma, anatafutwa na ndugu zake takribani wiki nne sasa baada ya kutoweka nyumbani kwake katika mazingira ya kutatanisha huku akiwa ameacha mke na watoto.

Akizungumza na Nipashe jana, dada wa Mwenge (51), Julieth Myangwila, alisema kaka yake alitoweka nyumbani kwake Agosti 2, mwaka huu, baada ya kupatwa ghafla na matatizo ya afya ya akili.

"Si kawaida yake kutoweka nyumbani lakini siku hiyo aliondoka bila kutoa taarifa, kama ndugu tumejaribu kumtafuta sehemu mbalimbali lakini hakuna mafanikio yoyote… tumeenda kwenye hospitali mbalimbali, vituo vya polisi, kwa ndugu zetu pamoja na vyumba vya kuhifadhi maiti lakini hakuna taarifa yoyote," alisema Myangwila.

Alisema baada ya juhudi zote kukosekana walitoa taarifa kituo cha polisi kati na kuandikiwa namba DOM/RB/10313/2022.

"Naomba mtu yeyote anayefahamu taarifa zake atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu au kwa kupiga simu 0679065621 (Pili) ama 0656490798 (Monica)," alisema.

# RC azitaka taasisi za fedha kuwasaidia wananchi kiuchumi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amezitaka taasisi za fedha nchini kushirikiana na serikali ili kuwainua wananchi kiuchumi.

Senyamule aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye hafla fupi ya Benki ya CRDB, kwa kutoa shukrani kwa wafanyakazi na wateja wao wa Kanda ya Kati kwa kuiwezesha kupata tuzo ya Euro Money nchini Uingereza, inayotolewa kwa benki bora Tanzania. Hafla hiyo ilifanyika katika Tawi la CRDB Dodoma.

Alisema, anatambua benki hiyo imekuwa na mchango mkubwa kwenye jamii lakini wasichoke waendelee katika kuwahudumia wananchi kwa njia zao mbalimbali.

Mkuu huyo wa mkoa aliipongeza CRDB kwa kupunguza riba ya mikopo kwa kundi la wakulima kwa sababu ilikuwa kero kubwa kwao kutokana na matatizo ya mabadiliko ya hali ya tabianchi yaliyotokana na mvua kuwa chini ya kiwango.

Aliitaka benki hiyo kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa makundi ya wajasiriamali, wamachinga, wafanyabiashara na wateja binafsi ili pato la taifa lizidi kuongezeka.

Kaimu Meneja wa CRDB Kanda ya Kati, Jane Maganga, alisema hafla hiyo iliwashirikisha baadhi ya wateja na wafanyakazi wa benki hiyo.

Maganga alisema lengo la hafla hiyo ni kuwashukuru kwa kuiwesha benki yao kupata mafanikio ya tuzo ya Euro Money nchini Uingereza kama benki bora Tanzania.

"Tunasherehekea mafanikio haya ambayo benki yetu imeyapata kwa kutunukiwa tuzo ya benki bora Tanzania inayotolewa na jarida maarufu la masuala ya fedha na uchumi la nchini Uingerezaa la Euromoney na tupo hapa kwa ajili ya hilo,"alisema Maganga.

Alibainisha kuwa tuzo hiyo ilipokewa na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Abdulmajid Nsekela wiki chache zilizopita jijini London.

Maganga alisema mafanikio hayo yamekuja kutokana na ufanisi wa kazi zinazofanywa na wafanyakazi hao pamoja na wateja wao wanaowaunga mkono katika huduma zinazotolewa hapo.

Pia alisema CRDB wamejikita zaidi katika kutengeneza thamani endelevu, kuongeza ujumuishi wa kifedha na kujenga uchumi jumuishi kupitia biashara, huduma na mifumo bunifu ya utoaji huduma.

Aidha, alisema wamekuwa wakifanya maboresho katika mikopo ya wajasiriamali hasa katika kipindi hichi ambacho dunia imepitia janga la UVIKO-19 kwa kushirikiana na washirika wa ndani na nje ya nchi.

Maganga alibainisha kuwa kwa mwaka jana pekee wamefanya uwezeshaji wa Sh. trilioni 5.4 kwa maana ya mikopo iliyotolewa kwa sekta zote.

Alisema jitihada hizo za kusaidia makundi mbalimbali nchini zimesababisha benki hiyo kufanya vizuri mwaka hadi mwaka ambapo katika kipindi cha miaka mitatu wateja wameongezeka kutoka milioni tatu hadi kufikia milioni nne.



# Surua yazidi kuongezeka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Elimu ya Afya katika Wizara ya Afya, Bakari Hamad Magarawa, amesema hali ya surua bado si shwari Zanzibar kutokana na kuwapo idadi kubwa ya wagonjwa.

Magarawa aliyasema hayo hayo jana mjini hapa wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya ugonjwa wa surua Zanzibar huku akibainisha kuwa hadi jana majira ya subuhi, kulikuwa na 316 huku Wilaya ya Magharibi B Unguja ikiongoza kwa kuwa na zaidi ya wagonjwa 200.

Alisema kuna vifo vitatu vilivyoripotiwa kwa mwezi huu vitokanavyo na surua, viwili vikitokea wilaya ya Magharibi B na kimoja Magharibi A Unguja.

“Bado ugonjwa wa surua unaendelea kuongezeka. Wilaya ya Magharibi B Unguja pekee ina zaidi ya wagonjwa 200, Magharibi A ina zaidi ya wagonjwa 70, wilaya ya Wete zaidi ya wagonjwa 40 na Chakechake, Pemba ndiyo wilaya pekee ambayo haijaripotiwa kuwa na wagonjwa wa surua,” alisema.

Pia alisema umri ambao unaathirika na ugonjwa wa surua ni watoto chini ya miaka mitano ingawa wako wagonjwa wachache wenye umri wa miaka 15 na zaidi ambao wameripotiwa kuwa na ugonjwa huo.

Kutokana na ongezeko hilo, aliwataka wazazi na walezi kuwapelekea watoto katika vituo vya afya kuwapatia chanjo ya surua ambayo inatolewa bure.

Alisema wagonjwa hao wa surua bado wanaendelea kupatiwa matibabu katika vituo mbalimbali vya afya.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema surua ni moja ya maradhi ya kuambukiza ambayo husababishwa na virusi aina ya ‘Morbillivirus paramyxvirus’ vinavyoelea kwa haraka kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya hewa au kugusa majimaji yatokanayo na mtu mwenye maambukizi.

“Ugonjwa huu huambukizwa pale mtu anayepata maambukizo ya vimelea hivi anapokohoa au kupiga chafya au kugusa sehemu zinazotumiwa na watu wengine,” alisema.

Hata hivyo, alisema ugonjwa huo huwaathiri watu wa rika zote lakini zaidi ni watoto chini ya umri wa miaka mitano, wajawazito na watu wenye upungufu wa kinga mwilini.

Aidha, alisema dalili za ugonjwa huo ni pamoja na homa kali, kukohoa, mafua na macho kuwa mekundu ambayo huambatana na vipele harara ambavyo hujitokeza katika paji la uso na hata mwili mzima pamoja na vidonda mdomoni au koo kuuma.

Waziri aliwaomba wananchi wanaopata dalili hizo, kufika vituo vya afya haraka ili kupata matibabu na kuwataka watumishi na wamiliki wa vituo vya afya kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa kuzingatia utekelezaji wa kulinda watumishi na watoa huduma.

Pia alisema wizara itaendelea kufuatilia mlipuko wa ugonjwa huo kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na washirika wengine wa maendeleo ili kuudhibiti haraka.

Kwa mujibu wa WHO, surua ni mojawapo ya sababu kuu za vifo miongoni mwa watoto wadogo ingawa chanjo salama na ya gharama nafuu inapatikana.

Mwaka 2015, kwa mujibu wa WHO, kulikuwa na vifo 134,200 vya surua duniani, takriban vifo 367 kila siku au vifo 15 kila saa.

Hata hivyo, chanjo ya surua ilisababisha kupungua kwa asilimia 79 kwa vifo vya ugonjwa huo kati ya mwaka 2000 na 2015 duniani kote.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (katikati), akizungumza na mawaziri, makatibu wakuu na watendaji wa taasisi zinazosimamia raslimali ya matofali ya mawe na mchanga, kuhusu kupata njia bora za matumizi na uhifadhi wake, ofisini kwake Migombani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapongezwa mwitikio chanya sensa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wa Wilaya ya Kusini Unguja wamepongezwa kwa mwitikio wao mkubwa wa Sensa ya Watu na Makaazi pamoja na ushirikiano wanaoutoa kwa makarani katika mchakato huo unaoendelea nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Rajab Yussuf Mkasaba, aliyasema hayo kwa nyakati tofauti alipofanya ziara ya kuangalia maendeleo ya sensa katika shehia mbalimbali za wilaya hiyo.

Katika ziara yake hiyo, Mkasaba aliwapongeza na kutoa shukurani kwa wananchi wa wilaya hiyo kwa kujitokeza kwa wingi na kuwapa ushirikiano makarani wa sensa, hatua ambayo inawarahisishia kufanya shughuli zao.

Alisema hatua hiyo inatoa faraja kwa wilaya na mkoa wa Kusini Unguja kwa kuona kwamba mafanikio makubwa zaidi yatapatikana pamoja na kufikia lengo lililokusudiwa na kwamba hatua hiyo ndiyo chachu ya maendeleo endelevu ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kujua idadi ya wakaazi wote nchini.

Mkasaba alitoa wito kwa wananchi wote ambao bado hawajapata fursa ya kuhesabiwa, kuendelea kuwa na subira na makarani kwa kuwa watahakikisha wananchi wote wanapata haki yao ya kuhesabiwa popote walipo kama walivyoahidiwa na serikali.

Nao masheha wa wilaya hiyo kwa nyakati tofauti, walieleza sensa hiyo inavyoendelea kwa mafanikio makubwa sambamba na kuwapo kwa amani, usalama na utulivu mkubwa.

Walisema kazi hiyo inakwenda vizuri pamoja na ushirikiano mzuri wanaoupata kutoka kwa wananchi hali ambayo inawarahishia kwa kiasi kikubwa kufanikisha shughuli zao hizo kwa ufanisi zaidi.

# Rais aiomba Oman msaada wa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiomba serikali ya Oman kusaidia upatikanaji wa mafunzo kwa watendaji wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa ya Oman, Dk. Hamed Mohd Al-Dhawiani, aliyefika nchini kwa lengo la kuendeleza ushirikiano kati ya nchi mbili hizo, hususan katika suala la uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za taifa.

Alisema kuna umuhimu kwa Oman kusaidia upatikanaji wa mafunzo kwa watendaji wa taasisi ya nyaraka na kumbukumbu Zanzibar ili kuwajengea uwezo.

Hatua hiyo, alisema itawawezesha watendaji hao kufanya kazi kwa weledi na ufanisi, hususan pale Zanzibar itakapofanikiwa kuwa na kituo cha maonyesho.

Aidha, alisema Zanzibar iko tayari kuendeleza uhusiano na ushirikiano na Oman katika uimarishaji wa hifadhi za nyaraka na kumbukumbu ziliopo ili kufikia kiwango cha kuwa na kituo cha maonyesho kama ilivyo kwa miji ya Lamu na Mombasa, nchini Kenya.z

Alisema mafanikio hayo yatasaidia uhifadhi bora wa historia ya Zanzibar, hususan kwa watu wanaokuja kujifunza au kufanya utafiti mbalimbali.

Naye Dk. Al- Dhawiani alisema, katika kuendeleza ushirikiano na Zanzibar, Oman imetenga bajeti maalum kwa ajili ya kusaidia uwekaji wa mazingira bora katika maeneo ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu zilizopo, huku akibainisha umuhimu wake katika kusaidia watu wenye mahitaji ya kufanya utafiti.

Alisema pia Oman inalenga kuendeleza programu ya kuwapatia mafunzo watendaji wa taasisi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kiutendaji.

Oman, alisema ina uzoefu mkubwa katika suala la uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu, ambapo watendaji kutoka mataifa mbalimbali duniani yakiwamo ya bara la Afrika wamekuwa wakifika nchini humo kwa ajili ya kujifunza.

Alisema Oman haina dhamira ya kuhodhi nyaraka ama kumbukumbu zilizopo hapa nchini na kusema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kusimamia nyaraka zake.



**HAMISA MOBETO**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT

JUMAMOSI AGOSTI 27, 2022

# JUMA JUX

## Mtanashati anayewatoa udenda wanawake



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Juma Jux, ameibua mjadala katika mitandao ya kijamii baada ya picha yake yenye utata kusambaa kwa kasi.

Nyota huyo wa miondoko ya pole maarufu kama R&B, hana kawaida ya kufanya mambo yanayoshangaza, lakini safari hii amekuwa midomoni mwa wengi kutokana na picha hiyo kutafsiriwa tofauti.

Hata hivyo, Jux ambaye jina lake kamili Juma Musa Mkambala, amesema picha hiyo amepiga kama tangazo la nguo za ndani ambazo zinajuimuisha bidhaa zake za nguo.

Baadhi ya watu walimshambulia vikali kwa kueleza kimsingi haleti taswira nzuri hasa kutokana na tabia yake ya ukimya na kupenda utanashati unaozingatia maadili.

**NANI JUMA JUX?**

Juma Jux amezaliwa Septemba 1, 1989 na kukulia katika jiji la Dar es Salaam.

Mwaka 2005 alianza harakati za muziki kama rapa na ilipofika 2008 alikutana na Cyril Kamikaze na Nigga flow wakatengeneza kundi la WAKACHA na kuwa na cheo cha makamu wa rais.

Hata hivyo, mwaka huo huo alisaini mkataba kujiunga na lebo ya AM Records, huko alibadili mwelekeo na kuanza kuimba nyimbo za kimahaba ambazo zilimtambulisha kwa mashabiki.

Kupitia miondoko hiyo, Jux amekuwa akipanda kila siku kwa kutoa nyimbo kali kama Sugua aliyomshirikisha Diamond Platnumz, Juu, Unaniweza, Upofu na nyingine.

**BIASHARA YA MAVAZI**

Jux anakuwa msanii pekee aliyefanikiwa katika biashara ya mavazi kupitia lebo yake ya 'African Boy' ambayo imekuwa maarufu ndani na nje ya nchi.

Kupitia biashara hiyo, amekuwa akijikusanyia mamilioni ya pesa, huku mwenyewe akishiriki kubuni na kutangaza bidhaa zake.

**UHUSIANO WA KIMAPENZI**

Unaweza kusema ni mmoja wa wasanii wachache nchini wanaopendeza kimtazamo kutokana na mwili wake kujengeka vyema na tabia yake ya kupenda utanashati.

Kutokana na mwonekano wake, kila mwanamke anatamani kuwa naye, lakini kwa Jux amekuwa tofauti kwani uhusiano wake kimapenzi umeufanya kuwa wa kawaida.

Hata hivyo penzi lake na mwanamuziki mwenzake Vanessa Mdee, lilikuwa gumzo kiasi cha kuonekana kama mfano kwa wengine. Hata hivyo waliachana na kila mtu amekuwa na maisha yake.

BASI SAWA

## Coy unayosema yasije yakakugeukia



MCHEKESHAJI na mwanzilishi wa jukwaa la Cheka Tu, Coy Mzungu, amesema nafasi aliyopewa Diamond Platnumz kuwaongoza, anaweza kuondolewa pale kunapotokea hitilafu.

Hivi karibuni Diamond, ambaye ni staa wa muziki wa Bongo Fleva na Mkurugenzi wa Wasafi Media, ameandika kupitia ukurasa wake wa kijamii kwamba kwa sasa ni CEO wa Cheka Tu.

Hata hivyo, Mzungu amesema nafasi hiyo haimpi dhamana ya yeye kuwa mmiliki wa Cheka Tu na mara nyingi CEO huwa mwajiriwa kwenye kampuni lakini mwanzilishi ndio mmiliki.

## Wasanii wa kike waomba kusaidiwa

MTANDAO wa wasanii wanawake Tanzania, kupitia mradi wake 'Tuseme Tusichoke' umeishauri serikali kuwekeza zaidi katika kuwainua wasanii wanawake waliopotea katika tasnia hiyo kufuatia janga la Uviko-19. Ushauri huo umetolewa na Mkurugenzi wa



Mtandao huo, Agnes Lukanga, wakati akielezea vikwazo vitano ambavyo wasanii wa kike walikumbana navyo.

Alisema, katika kipindi hicho wasanii wengi wa kike walikutana na vikwazo vingi ambavyo vilisababisha baadhi yao kushindwa kusimama kuendelea na kazi.

"Kuna mambo matano ambayo tumeyabaini yalikuwa vikwazo kwa wasanii wa kike ikiwamo kufanyiwa ukatili kwa baadhi yao, kutolipwa kwa pesa kwa baadhi ya wasanii wanapomaliza kufanya kazi kwa kisingizio cha corona," amesema.



## Mobetto mapenzi sawa na upupu

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Hamisa Mobetto, amesema kamwe haogopi kuibiwa mwanaume kutokana na kila kitu kinapangwa na Mungu.

Amesema, maneno ya watu kwamba anamficha mpenzi wake kwa kuhofia kuchukuliwa na wanawake wengine, haliingii akilini kwani mwanaume si kiumbe wa kufichwa bali anafanya hivyo kutokana na heshima.

"Mimi siamini sana mapenzi ya kila mmoja afahamu, unawapa nafasi watu kuacha kukufuatilia badala yake kuangazia mapenzi. Halafu mimi ni mama wa watoto wawili sio vizuri kila mwanaume ninayekuwa naye wakamjua," amesema.

## Siku Saba: Siyo siku ya mahaba

**Na Adam Fungamwango**

'SIKU Saba' ni filamu inayoonyesha na kuwakumbusha watu kuwa siku zote kikulacho ki nguoni mwako. Wa kale walioleta msemo huo wakiwa na maana kuwa siku zote anayekudhuru ni yule anayekujua. Hii inatufundisha kuwa mtu unapopata na matatizo angalia kwanza waliokuzunguka na wanaokupa sana pole, siyo wale ambao wewe unadhani adui zako. Mara nyingi watu wanapopatwa na matatizo wanayoletwa na binadamu huanza kuwadhania waliosababisha hivyo ni maadui zao. Wakati mwingine sivyo.

Imechezwa na Ally Makoroboi, Amina Badi, Omari Mbala, Rachel Mwanange, Abdallah Sultani na wengineo.

Salim na mkewe Zuhura wanaishi kwenye kijiji kimoja hapa nchini. Siku moja Zuhura hakuonekana nyumbani siku nzima. Mumewe anamsaka na kumfuma yupo kwa mpenzi wake wa zamani Sultani.

Sultani alikuwa ni mpenzi wa Zuhura kabla hajaolewa na Salim. Jambo hilo limamchukiza Salim na kugombana na Sultani.

Ikawa ni jambo la kawaida kwa Zuhura kutoweka nyumbani na akisakwa anakutwa kwa Sultani.

Salim alimpenda sana mkewe, hivyo alikuwa anamsamehe karibuni mara nne.

Hata hivyo jambo hilo linaleta ugomvi mkubwa baina ya Salim na Sultani, huku anayeiba wa mwenzake akimwambia mwenyewe kwa jeuri kuwa asali haiwezi kuonjwa mara moja.

Jambo hilo linamfanya Salim kwenda kumwambia kaka yake Mussa, ambaye anajitolea kwenda kumpiga Sultani. Hata hivyo hakufanikiwa.

Zuhura anatoweka nyumbani kwa mara ya nne. Mume anajua ni yale yale. Hata hivyo siku tatu zinafika hajarudi nyumbani. Salim anashtuka na kwenda kumwambia shemeji yake ambaye ni dada wa mkewe.

Kijiji kizima kinadhani kuwa huenda yupo kwa Sultani. Bado hakupatikana. Sultani naye anamfuata Salim, pamoja na kwamba



wana ugomvi lakini kwa jambo zito kama hilo ilibidi wapange mkakati wa kumsaka.

Sultani anamshauri Salim kwenda kuangalia kwa waganga wa kienyeji. Shemeji yake naye amwambia hivyo hivyo.

Wanafika kwa mganga, ambaye anafanikiwa kumrejesha Zuhura. Mganga anadai kuwa alichukuliwa kimazingira. Na lengo ilikuwa ni kuchukuliwa kizazi. Alitakiwa kukaa huko siku sita, siku ya saba anachukuliwa kizazi na asingeweza kuzaa tena. Bahati nzuri wamewahi. Anakabidhiwa mkewe, lakini anapewa dawa amwage uwanjani ili amfahamu mbaya wake.

Anayeanguka uwanjani hapo ni kaka yake Mussa. Alipomuuliza mganga akaambiwa huyo ndiye mbaya wako.

Mussa anakiri kumfanyia dawa shemeji yake, akamchukua kimazingara akishirikiana na mganga mmoja nje ya kijiji kwa ajili ya kumtoa kizazi na kumwekea mkewe ili azae nao wapate mtoto.





## Aslay akumbuka mengi mazito

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Aslay, wiki hii amewashtua mashabiki zake baada ya kuweka wazi kwamba ameweka saini mkataba wa kuwa chini ya lebo ya RockStar4000.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Aslay amesema kwamba kwake imekuwa safari ndefu yenye matumaini makubwa katika kusimamia kazi zake za muziki.

"Nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kipindi chote ambacho nilikuwa kimya, hakika nimejifunza Mengi," amesema Aslay.

## KALI 5 'LOVE SOUNDS' YA BARNABA

**Na Adam Fungamwango**

Ni hivi majuzi tu msanii mkongwe asiyechuja wa muziki wa Bongo Fleva, Barnaba, amezindua bonge la albamu alilolipa jina la 'Love Sounds Different' yenye ngoma 18 ndani yake.

Ni albamu yenye ngoma kali ambazo amezipiga kwa mitindo tofauti, akiimba na wasanii tofauti kiasi cha kutofautisha ladha ya wimbo huu na huu.

Hata hivyo leo tutaziangalia ngoma kali zaidi ambazo zimetokea kupendwa na mashabiki wake na wa muziki kwa ujumla kutokana na uimbaji wake, mapigo, pamoja na ubunifu wa wasanii aliowashirikisha.

**Hadithi- Ft Diamond Platnumz**

Ni ngoma ambayo imeonekana kufuatiliwa na kusikiliza zaidi. Labda kwa sababu amemshirikisha msanii maarufu zaidi nchini, Diamond Platinumz.

Kwenye ngoma hii, Barnaba na Diamond wamefanya balaa. Jamaa kwenye ngoma hii anamsifia mpenzi wake kuwa amefundishwa kumliwaza mume.

Kuna maneno ya nyimbo za watoto wa zamani walizokuwa wakiziimba usiku, wakisubiri ubwabwa na maharagwe nyumbani.

"Longa nisilonge, mwenzenu mimi, mchumba wangu, mmh, basi sisemi..."

**Sijiwezi-Ft Jux**

Inawezekana kabisa ukawa ni wimbo uliopigwa kwenye mahadhi ya kimapenzi zaidi kuliko nyimbo zote kwenye albamu hii.

Mapigo ya kubembeleza, kusikitisha na sauti murua zinazoendana, zinazolia na kudeka.

Umepigwa kwa mtindo wa taratibu. Amemshirikisha Jux. Jamaa anamwambia mpenzi wake kuwa hajiwezi. Kijana amefichwa ndani, lakini anajisifia. Anamwambia mpenzi wake mapenzi yamemchanganya kwa sababu amezidisha dozi na anampa uchizi.

**Hunitaki Ft Mbosso**

Ni wimbo ambao amemshirikisha Mbosso. Jamaa analilia mapenzi. Alichana na mpenzi wake, lakini bado anamkumbuka. Anaonekana kama kutaka kurudisha majeshi, lakini demu kakomaa.


"Nakutumia meseji hujibu, 'fine', ukiniona hunisalimii 'fine', ukiniona unabadili njia 'fine'", jamaa analalamika." Bado anamkumbusha, bado anamuota. Ndiyo inavyokuwa, unayempenda yeye hakupendi.

**Wahoroni Ft Yong Lunya**

Hii ni ngoma ambayo imechanganya ladha. Ina R&B na Hip Hop. Kama kawaida Barnaba anaimba na Young Lunya yeye anarap,

"Kama kitandani tuwe wote, na kaburini pia tuwe wote, hakuna mimi bila wewe..." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

**Cheketua Ft Ali Kiba**



Hii sasa amemshirikisha Ali Kiba na ngoma yenyewe ilivyopigwa unaweza ukadhani labda ya Kiba. Mashabiki wanajua kuwa msanii huyo ngoma zake zina mapigo fulani hivi ya kuchangamsha na magitaa kama kina Koffi Olomide, Fally Ipupa na Fere Gola. Kwenye wimbo huu kuna baadhi ya maneno haya.

"Nikupe habari tangu nirudi safari, nikakupata kimwali, tumeshinda zohari. Nitazungumza na bibi na babu wataridhia, shela wigi, mie kanzu na jambia."



# Nick kweli umekuja kuijaza dunia

MWIGIZAJI na mwendeshaji wa kipindi cha televisheni, Nick Canon, amesema anatarajia kupata mtoto wa kumi hivi karibuni.

Katika ukurasa wake wa Instagram, amewaambia mashabiki zake kwamba mpenzi wake Brittany Bell ndiye amebeba ujauzito wa mtoto huyo.

Nick aliandika, "Muda utasimama kwa kitakachotokea, Brittany anatarajia kunipa mtoto mwingine kama zawadi," ameandika.



## Portabo kalianzisha tena

WANIGERIA wamejikuta wakimjadili rapa Portable, ambaye hivi karibuni ameibua utata mwingine akitambulisha kama kiongozi wa eneo la Tigbo Awori.

Msanii huyo aliyetoka katika maisha ya mitaani, aliweka video fupi katika ukurasa wake wa Instagram akionekana akitawazwa katika cheo hicho ambacho kinatolewa na Serikali ya Mitaa ya Yewa katika Jimbo la Ogun.

Katika video hiyo, Portable alionekana akipokea hadhi yake mpya kutoka kwa mfalme wa eneo hilo ambaye alimtangaza kama msafishaji mkuu wa furaha ya Ardhi ya Tigbo Awori.

## Eedris afanyiwa upasuaji wa figo

TAARIFA zilizopatikana kutoka kambi ya rapa mkongwe nchini Nigeria, Eedris Abdulkareem, zinasema kuwa upasuaji wa figo aliofanyiwa hivi karibuni ulikuwa wa mafanikio.

Msanii huyo mwezi uliopita, iliripotiwa kwamba ni mgonjwa kutokana na figo kushindwa kufanya kazi.

Baada ya tangazo hilo, mwanamuziki M.I Abaga alikuwa wa kwanza kuwataka watu kumwombea na kumpatia msaada.





## Duh! Buju kabadilisha gia angani

MWIMBAJI wa Nigeria Buju BNXN, ambaye anatuhumiwa kumtemea mate ofisa wa polisi, amebadili gia angani baada ya kusema suala hilo linakuzwa na watu na kwamba kamwe hawezi kufanya unyanyasaji wa aina hiyo.

Msanii huyo ambaye aliitwa polisi kwa mahojiano alianzisha sakata hilo, baada ya kuandika kwenye mtandao wa kijamii kwamba alimtemea mate polisi akiwa uwanja wa ndege.

"Twitter yangu niliifuta tangu niliposema maneno ya kipuuzi, nilimkosea heshima ofisa wa polisi na sio jinsi watu walivyochukulia kwenye mitandao ya kijamii. Siungi mkono vurugu au unyanyasaji dhidi ya polisi kwa namna yoyote ile," alitweet.

## Davido siasa na wewe wapi na wapi

MWIMBAJI mashuhuri wa kimataifa, David Adeleke, anayejulikana Davido, amemjia juu mgombea wa Chama cha APC, ambaye awali alimkejeli kuhusu kesi za mjomba wake, Ademola Adeleke.

Kumbuka kwamba Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (INEC) ilimtangaza Adeleke kuwa mshindi wa uchaguzi wa ugavana Julai 16 katika Jimbo la Osun akiwa amepata jumla ya kura 403,271 dhidi ya 375,027 zilizopigwa na Gavana Oyetola.

Davido amesema wacha watu wapige kelele lakini ukweli ni kwamba mjomba wake ameshinda kihalali na kama wanapinga waende mahakamani.



MAKALA

# Wanawake wanavyopitia machungu ya uongozi

## ■Wengi walazimishwa rushwa ya ngono

Na Mwandishi Wetu

VIKWAZO vinavyowazuia wanawake kukosa nafasi za uongozi kutoka ngazi za chini hadi juu vimetajwa kuwa ni rushwa ya ngono na kiuchumi.

Kauli hio imetolewa na wanachama wa vikundi mbalimbali vya vya wanawake jijini Dar es Salaama vikiwamo vya ujasiriamali na siasa walipokutana kwenye mafunzo ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi.

Mafunzo hayo yalioandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipinguni, na kuwashirikisha wanawake zaidi ya 40 kutoka kata za Majohe na Kipunguni.

Asia Ally, ambaye ni mjumbe wa serikali ya mtaa wa Amani, anasema rushwa, pesa, na ngono imekithiri kwenye vyama vya siasa, na imekuwa kikwazo kwa wanawake kushiriki katika siasa.

Anajitolea mfano kwamba yeye mwenyewe alikumbana na tukio la kulazimishwa kufanya ngono na kiongozi, lakini alisimama imara na kuishinda wakati akiwania nafasi ya udiwani wa Kata ya Bolisa, wilayani Kondoa mkoa wa Dodoma.

"Jambo la muhimu ni kujiamini, kwani bila kuwa na msimamo, unaweza kutumika kwa manufaa ya wengine na hatimaye unabaki kama ulivyo bila kupata nafasi ya uongozi katika chama," anasema Asia. Akifafanua zaidi, anasema aliambiwa na mmoja wa wajumbe wa vikao vya mapendekezo ya majina ya wagombea kuwa atoe rushwa ya ngono ili jina lake lipitishwe kuwakilisha chama.

"Sikukubali mchezo huo mchafu, nilisimama imara ingawa sikushinda, nilikuja Dar es Salaam nikashinda ujumbe wa serikali ya mtaa, na sasa nina mpango wa kuwania nafasi ya mwenyekiti wa mtaa uchaguzi ujao," anasema. Mjumbe huyo anasema, wapo wanaokubali kutoa rushwa hiyo na kupata uongozi na wengine hutoa na kukosa.

Anaongeza kwamba, njia nzuri ni kuikataa, kwa kuwa inadhalilisha utu wa mwanamke.

kauli hiyo inaungwa mkono na mwanamke mwingine Asha Dingale, ambaye anadai kuwa alishawahi kuwania udiwani wa Kata ya Malumbo Kisarawe mkoani Pwani na kukumbana na kikwazo hicho.

"Nililazimika kujiondoa katika kinyang'anyiro ili nisiingie katika mtego. Kwanza anayekuomba rushwa hiyo hawezi kukusaidia kupata nafasi kwa sababu jina halipitishwi na mjumbe mmoja, hivyo ni muhimu wanawake kuendelea kuipinga kwa nguvu zetu zote," anasisitiza Asha.

Hata hivyo, makamu mwenyekiti wa kampeni ya Shujaa wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii Mkoa wa Pwani (SMAUJATA), Shemsuu Issaya, anawataka wanawake kutokuwa chanzo cha ushawishi wa rushwa ya ngono katika siasa na maeneo mengine, badala yake wawe chachu ya kukemea.



Makamu Mwenyekiti wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii Mkoa wa Pwani (SMAUJATA), Shemsuu Issaya (kulia), akichangia mada kwenye semina hiyo.

Anasema, baadhi ya wanawake huchangia kuwapo kwa rushwa hiyo katika siasa na maeneo mengine ikiwamo kwenye ajira na elimu kwa kuvaa mavazi ya mitego yanayosababisha wanaume washawishike kuwatamani.

"Tuache mtindo wa kutengeneza mazingira ya rushwa ya ngono kwa mavazi ya mitego, badala yake tujiheshimu na kuwa majasiri wa kukemea rushwa hiyo ndani ya jamii ili tusiendelee kudhalilishwa," anasema Shamsuu.

Shamsuu, anaeleza kuwa wanawake wana uwezo wa kuongoza, na kwamba hakuna haja ya kutumia mavazi ya mitego ili kutafuta uongozi, ajira na elimu.

"Tukumbuke mtoa rushwa na mpokea rushwa wote wana makosa, hivyo katika semina hii ni muhimu kila mmoja wetu kutoka akiwa ameiva na kwenda kusaidia wenzake kutokubali kudhalilishwa," anasisitiza

Anasema, haipendezi kuona ndani ya vyama vya siasa, wanawake wanadhalilishwa ma kuonekana kama si binadamu.

"Ninajua kuna kikwazo cha kiuchumi, lakini kwa semina hii ambayo pia tumejifunzia ujasirimali, ninaamini tunaweza kujiimarisha kiuchumi na hata tunapowania uongozi tuwe na uwezo, fedha zetu badala ya kutegemea wanaume ambao mwisho wa siku wanatudhalilisha," anasema.

**KAULI YA SAUTI YA JAMII**

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, anasema mafunzo hayo yalilenga kuwasaidia wanawake kuendesha shughuli zao za kiuchumi, ili wasinyanyaswe kwenye Nyanja ya siasa na hata katika mazingira mengine kwa ukosefu wa kipato.

"Mambo mengi yakiwamo ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia, yanatokea kutokana na ukosefu wa kipato, hivyo, Women Fund wametuwezesha, ili tusaidie wanawake na wasichana kuepuka hayo," anasema Bishagazi.

Anaongeza kuwa baadhi ya wanawake wanakumbana na vikwazo, anaamini kupitia semina hiyo watatoka wakiwa wanatambua haki zao za msingi na kushinda rushwa hiyo na ukatili mwingine.

Bishagazi anaongeza kuwa kwenye rushwa ya ngono, baadhi ya wanawake huwa hawatoi taarifa kwa kuogopa unyanyapaa na kwamba wamewaelekeza jinsi ya kutoa taarifa katika vyombo husika ikiwamo Takukuru.

"Rushwa ya ngono si ajali bali ni mchakato, hivyo ni rahisi kutoka taarifa wakati mchakato ukiendelea, mhusika akamatwe haraka, ili kukomesha vitendo hivyo katika jamii yetu," anasema.

Anasema, ipo haja kwa jamii kupaza sauti, kwa kuwa rushwa ya ngono inaua, inapoteza utu, inaleta msongo wa mawazo na kuhujumu uchumi.

" Niwashukuru Women Fund Tanzania, kwa ufadhili wao, nasi tutaendelea kuelimisha umma wa Watanzania hasa wanawake kujua haki zao na kuwa tayari kukwepa rushwa hiyo," anasema.

Bishagazi, anasema rushwa ya ngono ni janga kwa nchi na kutaka kuwako na mikakati madhubuti na ya ubunifu kuhakikisha inakoma.




Mkurugenzi wa Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Biashagazi (kushoto), akitoa elimu kuhusu haki za wanawake. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...



Na Adam Fungamwango

# Unakumbuka enzi za mchele kitumbo?

## ■VIP, cherekochekero, mdundiko, ulitikisa
## ■Vituko siku ya kula wali



MWANZONI mwa miaka ya 1990 kurudi nyuma, wali au ubwabwa ulionekana ni chakula cha kifahari sana kwa Watanzania. Naambiwa kuwa siyo Tanzania tu, bali Afrika nzima wali uliliwa na watu kwenye kada za juu.

Lakini Tanzania ilikuwa zaidi, hasa pale nchi ilipotoka kumaliza Vita ya Uganda ambapo nchi ilikuwa kwenye hali mbaya ya uchumi na kutoka tamko 'Watanzania tufunge mikanda'.

Kwa kawaida, Waafrika wengi hususan Watanzania, chakula kikuu ni ugali, sasa hapo inategemea na maeneo kwani kuna sehemu wanakuwa wa mahindi, kwingine mtama, ulezi na nafaka nyingine.

Kiasili kabisa mchele si chakula kikuu kwa Waafrika, bali watu kutoka bara la Asia.

Historia inasema mbegu ya mpunga ililetwa nchini kutoka Asia na waliokuwa wanafanya biashara za utumwa mwaka 1868.

Hata hivyo, chakula hicho kimekuwa pendwa kwa Watanzania wengi na hii kwa sababu kimekuwa hakipikwi mara kwa mara, hasa wakati huo.

Kutokana na maendeleo ya kilimo na nchi kwa ujumla, kwa sasa familia hata za chini zina uwezo wa kupata au kununua mchele na kula kila siku, wakitaka wanaweza kula asubuhi, mchana na jioni. Zamani haikuwa hivyo.

Hata shuleni kwenye mabweni, wali hakikuwa chakula kilichokuwa kinapikwa kila siku.

Miaka hiyo ulikuwa unapikwa na kuliwa kwenye shughuli maalum tu, kama sherehe na matukio ya kijamii na sikukuu mbalimbali kama Idd El Fitri, Krismasi na Mwaka Mpya.

Hata leo hii wali hupendwa zaidi kwenye mikoa ya ukanda wa Pwani na maeneo jirani. Na hii inatokana na historia kwani Waarabu walioleta zao hilo na ndiyo chakula cha kikuu walipendelea kuishi maeneo ya Pwani kama Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Kilwa, Pwani, Zanzibar na sehemu zingine za mwambao.

Kutokana na kwamba wakati huo wali au ubwabwa hakikuwa chakula cha kawaida kwenye familia mbalimbali, siku ukipikwa utajua tu.

Kwanza kabisa watoto wanakuwa na furaha muda wote. Hata wale ambao ni wavivu kuoga siku hiyo wataoga mapema, bila shinikizo lolote kutoka kwa mama au mzazi.

Na katika kile kinachoonyesha hakikubwa chakula cha kawaida wakati huo, huwezi kukuta wali unaliwa mchana.

Unaweza ukadhani kuwa ni sheria, utaratibu au utamaduni, wali ulipikwa jioni tu.

Sehemu ambayo kaya siku hiyo haikupika wali ilipoonza. Watoto walijisikia vibaya. Hawakuwa na raha. Lakini sehemu ambazo 'wanakula mpunga' siku hiyo watoto watacheza, wataimba mpaka muda ambao wali unapakuliwa.

Na siku hiyo hata wale watoto ambao huwa na tabia ya kulala mapema, hakufanya hivyo.

Hii ni kuonyesha kuwa wali ni chakula ambacho wakati huo kilikuwa shida sana kupatikana.

Siyo kama Tanzania haikuwa inalipa mchele, ulikuwapo mchele wa Ifakara na Mbeya, moja ya mikoa inayolima mpunga na kutoa mchele ambao unasemekana ni wa kiwango cha juu nchini, lakini Vita ya Kagera ilisababisha chakula hicho kisitosheleze.

Kumbuka hadi leo hii, mchele kutoka Ifakara na Mbeya ndiyo huuzwa bei ya juu zaidi kuliko uliolimwa sehemu zingine za Tanzania.

Kina mama wenyewe wanajua anapokwenda kuununua, kwanza wananusa. Ni mchele ambao ukipika unanukia mpaka nyumba za jirani wakajua kama leo wanapika ubwabwa nyumba jirani.

Kutokana na uhaba wa chakula ikiwamo hata unga wakati huo, serikali ilibidi iagize kutoka nje.

Niliandika hapa jinsi Tanzania ilivyoletewa mahindi na unga wa rangi ya njano kutoka nchini Marekani kwa ajili ya kujikimu na uhaba wa chakula baada ya vita.

Hata mchele pia uliagizwa. Mchele uliagizwa kutoka Mashariki ya Mbali, bara la Asia na ulijizoelea umaarufu sana hapa nchini.

Wataalamu wanasema kuwa aina 235 za mchele duniani na huenda zikaongezeka kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Hata hivyo kuna aina maarufu za michele kama vile basmati, mchele bomba na aina tofauti, huku majina yakitolewa kutokana na mzingira husika.

Nchini Tanzania ilipoleta shehena ya mchele kutoka barani Asia, watu waliita kwa majina mbalimbali.

Kuna mchele maarufu wa kitumbo. Huu haukuwa umenyooka kama michele mingine, badala yake ulikuwa mfupi na kwa mbali ulionekana kama unataka kuwa wa duara. Ulituna kati na kutengeneza kitu kama tumbo, ndiyo maana ukaitwa mchele kitumbo.

Huu ndio ulipatikana kwa wingi na kipindi ambacho kulikuwa na uhaba wa chakula ndiyo uliokuwa wa gharama zaidi kuliko aina nyingine za mchele na ulikuwa na bei kubwa.

Mwingine ulikuwa ni VIP. Nao ulitoka barani Asia, lakini ulikuwa wenye hadhi fulani, hasa kwa wale ambao walikuwa hawaukubali mchele kitumbo. Wale walioutoa kasoro kitumbo ndiyo waliokuwa wanakimbilia kununua VIP. Halafu VIP ulikubaliwa sana kama ukipika pilau. Kifupi tu ni kwamba mchele kitumbo haikuwa na chuya kabisa, sasa baadhi ya watu wakawa wana wasiwasi nao kama ni kweli mchele wa kawaida au kuna namna. Kumbe ni ubora tu, kwa sababu hata leo tumeanza kuona michele ambayo haina chuya.

Mchele mwingine uliita mdundiko. Huu ulikuwa mchele wa hali ya chini, na uliuzwa bei rahisi. Ulionekana kama si mchele halisi bali chenga za mchele wenyewe, baadaye pia kinamama wakaupachika jina lingine chereko chereko.

**Tuma meseji 0716 350534**



Mchele wa kitumbo

## Wananchi wapewa hadhari mawakili vishoka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HAKIMU Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Edmund Kente, amewataka wananchi kuwa makini na mawakili 'vishoka' wanawatoza fedha nyingi kwa ajili ya kuendesha mashauri kinyume cha sheria.

Amesema mawakili hao pia wamekuwa chanzo kikubwa cha kuwafilisi wananchi wakati wa uendeshaji wa kesi na kuwataka kukata rufani Mahakama Kuu wakati kesi zao zimeisha salama na kuamuliwa kwa haki kwa mujibu wa sheria.

Kente aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake juu ya kuwapo mawakili 'vishoka' ambao wanaonekana kukithiri wilayani humo.

Alisema badala ya mawakili kuwasaidia wananchi wao wanawatoza viwango vikubwa vya fedha wakati wa uendeshaji wa kesi zao.

Hakimu Kente alisema mawakili hao wamekuwa na tabia ya wakiwashawishi wananchi walioshindwa kesi kihalali kukata rufani na kuendelea mahakama za juu ili hali wanafahamu hawana uwezo wa kuzisimamia na badala yake wanakuwa wanahitaji fedha kutoka kwao.

Kente alisema mawakili hao wanachukua fedha nyingi kwa wateja na wakati mwingine kuwaambia hata kuuza mali zao ili waweze kuwasaidia katika kesi zao ili hali wao hawatambuliki na serikali.

"Sisi tunashangaa wananchi wengi kuwaamini watu hawa kwanza hawalipi kodi na wanachukua fedha za watu kinyume cha sheria hali ambayo imekuwa ikiwasababishia wananchi umaskini katika familia zao," alisema Kente.

Alisema kuingia kwa mfumo wa kielektroniki katika mahakama umesaidia kupunguza mrundikano wa kesi na kusaidia mawakili 'vishoka' kutokupata nyaraka za washtakiwa hali ambayo imewafanya hata wao kupungua kutokana na kutokuwapo kwa mashauri mengi.

Kente aliwataka wananchi kama kuna tatizo lolote la kisheria wafike katika ofisi za mahakama kwani wao wapo kwa ajili ya kuwasaidia wananchi katika mambo mbalimbali yanayohusu sheria pamoja na kutoa ushauri.

# Waziri awa mbogo mradi kusuasua

**Na Happy Severine,**
BARIADI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameitaka Kampuni ya Afrihost Investment Limited inayojenga tangi la kuhifadhi maji katika mradi wa Malekano-Kadoto, Kijiji cha Mwang'handa, Maswa mkoani Simiyu kukamilisha kazi hiyo ifikapo Septemba 7, mwaka huu.

Ndaki alisema hayo jana katika kijiji cha Mwang'handa sehemu linapojengwa tangi hilo wakati akikagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika jimbo hilo.

Alisema mara kadhaa amekuwa akipita katika eneo la ujenzi wa tangi hilo, lakini amebaini mradi huo umekuwa ukisuasua jambo ambalo linawafanya wananchi kuchelewa kupata huduma ya maji katika vijiji vya Malekano, Kadoto na Mwang'handa.

Waziri Ndaki alisema chanzo cha maji kipo lakini mkandarasi ndiye amekuwa akichelewesha ujenzi wa tangi hilo na kwamba lisipokamilika wananchi hawatapata maji.

"Chanzo cha maji kipo kwa taarifa za wataalamu, maji yapo ya kutosha lakini anayetuchelewesha ni huyu mkandarasi ambaye kazi zake ni za kusuasua.

"Mwambieni huyo mkandarasi ambaye hayupo hapa na ametukimbia kuwa ifikapo Septemba 7, mwaka huu, awe amekamilisha hii kazi kwa mujibu wa mkataba wake kinyume cha hapo aondoke kwani pesa kapewa bado anafanya mchezo mchezo mie sitakubali," alisema.

Kwa mujibu wa Ndaki, serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji lakini baadhi ya makandarasi waliopewa kazi za kujenga miundombinu ya maji, wamekuwa wakichelewesha kazi walizopewa, hivyo kuwachelewesha wananchi kupata huduma ya majisafi na salama.

Awali, Kaimu Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Maswa, John Jishuli, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, alisema mradi huo ambao uko chini ya RUWASA ukikamilika, utahudumia wananchi wa vijiji hivyo na gharama ya ujenzi wake ni Sh. milioni 716,6.

Meneja huyo alisema mradi huo ulianza Machi 7, mwaka huu, na ulipangwa kukamilika ifikapo Septemba 7, mwaka huu.

Alisema hadi sasa mkandarasi huyo ameshalipwa kiasi cha Sh. milioni 913 na kazi ambazo zimepangwa kufanyika ni pamoja na ujenzi wa vituo 8 vya kuchotea maji, ujenzi wa tenki lenye mita za ujazo 135 pamoja na kuchimba mtaro wa kuweka bomba la mtandao wa maji kwa kilimo 11.

"Mradi huu utahudumia watu 4,000 katika vijiji vya Malekano, Kadoto na Mwang'handa na chanzo cha maji ni kisima kirefu kilichoko kwenye kijiji cha Malekano ambacho kina chake ni mita 70," alisema.




Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada (kulia), akimpongeza Naibu Meya mpya Julie Sawani, ambaye ni Diwani wa Kata ya Kihesa, baada ya kuchaguliwa kwa kura zote katika mkutano wa Baraza la Madiwani la mwaka kujadili taarifa za utendaji na uwajibikaji wa halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Serikali yajipanga kuyatokomeza magonjwa yasiyopewa kipaumbele

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imesema inakusudia kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele yakiwamo matende na mabusha, vikope, kichocho, minyoo na usubi ifikapo mwaka 2030.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Yunus Mgaya, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ufunguzi wa mkutano wa 10 wa kutengeneza mpango kazi wa mwaka 2022/23 wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Mgaya alisema lengo kuu la mpango huo ni kutokomeza kabisa magonjwa hayo kule ambako yanaendelea kutokea.

"Wizara ya Afya imeendelea na mpango mkakati wa kusambaza kingatiba kwa wananchi wote, ili kudhibiti magonjwa hayo, tunaamini tukiendelea hivi, ikifika mwaka 2030 tunaweza tukawa tumepunguza magonjwa kwa kiasi cha kutangaza kwamba Tanzania magonjwa haya sio tena mzigo katika mfumo wa afya," alisema.

Prof. Mgaya alisema mkakati wa kutoa kingatiba umewezesha kupunguza magonjwa, katika sehemu mbalimbali za nchi na kwamba wilaya nyingi ambazo zilikuwa na matatizo haya sasa hivi hakuna.

"Zimebaki wilaya chache, kwa mfano ugonjwa wa matende na mabusha tumebaki na wilaya tisa, ambazo ni pamoja na Ilala, Kinondoni, Temeke, Mtama, Lindi, Mafia, Kilwa, Pangani na Mtwara Mikindani," alisema.

Pia aliwataka wananchi kufuata maelekezo yote yanayotolewa na wataalamu wa afya na unapofikia wakati wa kutoa kingatiba zinazosambazwa, waendelee kumeza dawa kwa ajili ya usalama wa afya zao.

"Wizara imeweka nguvu kubwa, katika kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yameathirika na magonjwa haya, wananchi wake wanapewa kingatiba kwa ujumla, hivyo wito wangu ni kwamba wasiche kumeza dawa wanazopewa," alisema.

Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kimataifa (RTI) kutoka Marekani, Dk. Upendo Mwingira, alisema wamekuwa wakifanya tathmini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na wadau kutoka NIMR ili kujua kingatiba wanazozitoa zina matokeo gani.

"Hatua hiyo imesaidia kwani wilaya ambazo zimekuwa zikipewa kingatiba zimeshuka kutoka 119 hadi kufikia tisa, ambapo wilaya 110 zote hazina hatari ya maambukizi ya matende na mabusha nchini," anasema Dk. Mwingira.

Aliongeza kuwa taasisi hiyo kujikita katika kuboresha mifumo ya afya kwa kuangalia jinsi gani baada ya kugawa kingatiba kwa jamii na kuhakikisha magonjwa hayo hayarudi tena.

"Ni muhimu pia kuboresha mifumo, ushirikishwaji wa jamii katika kuelewa ili kutambua njia mbalimbali za kudhibiti magonjwa na njia zinazotumika ili ifikapo mwaka 2030 Tanzania iwe imetokomeza magonjwa haya," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDWARD PETER CHALAMILA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1247/0132** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **ST.MARK'S** mwaka 2007, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MBA/RB/278682/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ARNOLD KAKWEZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0731-0151** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MAKONGO mwaka 2004, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **URP/RB/1086/2015**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **SHABIRU HATIBU ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye namba za usajili **MC 425 DGB.** Yenye Chassis Na. **LDAPAJOB7NGB02002** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **MUH/RB/2431/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **SHABIRU HATIBU ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye namba za usajili **MC 707 DGE.** Yenye Chassis Na. **LDAPAJOB9MGB05465** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **MUH/RB/2431/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **SHABIRU HATIBU ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye namba za usajili **MC 532 CRM.** Yenye Chassis Na. **LDAPAJOB3LGB01619** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **MUH/RB/2431/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HEZRON DAVID MBISE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye namba za usajili **T 477 AND,** chasis namba **kzj 780001935,** engine namba **lkz0006466,** yeyote atakayeikokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/338966/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEO PLASTICS LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISHI yenye namba za usajili **T597 ARB,** chasis namba mmbjnkb407d064198,engine namba **4d56ucak6367,** yeyote atakayeikokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/338940/2022**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT COURT OF TANZANIA**
**AT ARUSHA**

**CIVIL/APPLICATION/CASE/NO…34..OF …2022**
**CHARLES MOLLEL & LUCAS MOLLEL PLAINTIFF/APPLICANT /D/HOLDER**

**VERSUS**

**OSIDAY LAIZER DEFENDANT/RESPONDENT/J/DEBTOR**
**NOTICE OF HEARING/MENTION**

**TO… OSIDAY LAIZER**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the District Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 5th day of SEPTEMBER 2022 at 08:30 am O'clook in the forenoon.
You may appeal in person or by Advocate or agent duly authorized to appeal on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE** That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.
GIVEN under my hand and the Seal of the court this **26th day of AUGUST 202**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
ARUSHA

**MWAMBA MILLENIUM COMPANY LIMITED**
**CHIMWAGA DODOMA**

**MNADA WA HADHARA**

KWA AMRI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KONDOA MJINI TUTAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA SHAMBA LILILOPO KATIKA KIJIJI CHA **ATA KATA YA KISESE** WILAYA YA KONDOA MJINI MALI YA NDUGU **HASSANI HAMISI SELEMANI** ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA **BI MWANAIDI NADA.** MNADA UTAFANYIKA TAREHE 02/09/2022 SAA TANO KAMILI (5:00) ASUBUHI

**MASHARTI YA MNADA: -**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
2. MALIPO 25% BEI ITAYOWEKWA KWENYE MNADA NA 75% ATAMALIZIA NDANI YA SIKU 14
3. ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOWEKWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZOTE
4. KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA KWA SIMU NAMBA **0712245977, 0627889248**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

## KUPOTEA KWA OFFER YA KIWANJA

**HUSNA S. MADABA** anatangaza kupotelewa na Offer ya Kiwanja **PLOT NO. 280 BLOCK "D" MAHUNGU, DODOMA CITY COUNCIL.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/337831/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PERPETUA KAKILLA MAGANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CORONA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T132 AWM.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH /RB/ 583 /2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA LUSHOTO.**

**YAH: MAOMBI NA.9/2022.**

Ubiri Village Council ambaye ni muombaji dhidi ya Hamis Samauva, Hidaya Salim Ngereza, Shamila Ramadhani, Ayubu Samauva, Salim Shetembo na Paula Kajoka, ambao ni wajibu maombi.

Popote walipo, Ubiri Village Council, amefungua shauri Na. 9/2022 mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Lushoto. Shauri husika limepangwa kutajwa Septemba 6, 2022 saa 3.30 asubuhi. Hivyo basi, mnatakiwa kuleta utetezi wenu ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Lushoto.

Endapo hamtotekeleza haya, shauri hili litatekelezwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yenu. Ofisi za Baraza zipo wazi karibu na jengo la Posta.

MWENYEKITI
T.E. CHINOLO
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
LUSHOTO

**KUITWA SHAURINI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MCA/63)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Muleba Mjini**
**Wilaya ya Muleba**
**Talaka madai no 11/2022**

**JAMHURI**
**Kwa Magreth Yunusu Nkolo**
**WA Izigo – Kaboya**
**K.K**
**Afisa Mtendaji**
**Kata Izigo**

Unaamrishwa na Jamhuri Uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya IJUMAA Tarehe 31/08/2022 asubuhi kuwa mdaiwa katika shauri lililoko mbele ya Mahakama hii ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya mahakama na unaonywa kwamba usipuuzie wito huu.
Ukipuuzia wito huu bila udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria.
Hati hii inatolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 4/08/2022
Kuitwa shaurini hii kwa maombi ya :-
Mpoki Nicodemu Kalulunga wa Kaboya

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MAYALA KATEMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T546 BZT.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH /RB/ 1156 /2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO WA MIRATHI NA 10 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA VICENT NDEMCHILIO MREMA….MAREHEMU**

**REV JAMES ALPHONCE IJIKO……MUOMBAJI**

**TAARIFA YAB KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29 mwezi agosti mwaka 2022
Imewasilishwa mwanga leo tarehe 15 mwezi agosti,mwaka 2022

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HASSAN MWAGA HASSAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye namba zza usajili T725 DRS, chasis namba **anh100012858,** engine namba **2az0964044,** yeyote atakayeikokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/337129/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DANIEL KONGU OLOIRUSHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LANDROVER** yenye namba za usajili **T961 AEH,** chasisi namba **lbcahiaf503591,** engine namba **902885756,** yeyote atakayeikokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/337064/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VERA BONAVENTRYRA SWAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye namba za usajili **T318 BEV,** chasis namba **gx1106008300,** yeyote atakayeikokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/337206/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA KIHONDA, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na……45/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: CHARLES MUSSA WA CHIEDU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA ABIHUDI CHARLES MUSSA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 31Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 08 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-20

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Ndiyo, mimi niko tayari kutoroka, nilikuwa tayari kuolewa, lakini kwa sababu umerudi na umesema kile ambacho hata mimi nilikuwa nacho rohoni, siwezi tena kuvumilia. Siwezi kuishi bila wewe. Na hapa ukinyanyua mguu na mimi naondoka. Tunaondoka wote."

"Hutaki tena ndoa?"

"Naitaka, lakini na wewe."

"Watu wameshatoa pesa zao lakini."

"Mbona wewe Bakari hueleweki? Si umeniambia kuwa unanipenda na unataka kunioa wakati ulikuwa unajua kabisa kuwa nimechumbiwa. Basi bora usingesema ili mimi niendelee na taratibu za harusi, ukasema 'nawasilisha ombi langu la kutaka kukuoa.' Sasa vipi, au ulikuwa unanijaribu?" Akauliza kwa hasira.

"Hapana mpenzi." Bakari akasogea na kumshika Siwatu. Kwa mara ya kwanza akamshika kama mpenzi wake halisi.

Siwatu alishusha hasira. Akafarijika. Kwa mara ya kwanza akahisi kitu ambacho hakuwahi kukihisi maishani kwake.

Kuitwa mpenzi kwa mara ya kwanza na Bakari kulimfanya ajisikia faraja. Akaangua kilio cha faraja kilichochanganyikana na huzuni.

Anampenda Bakari, lakini papo hapo hakujua afanye nini ili kuepuka kufunga ndoa na mwanaume mwingine ambaye hajawahi kumuona, lakini ni yeye mwenyewe ndiye alikubali kutokana na upweke.

*****************************

Wiki iliyofuata Billy na Daudi walirejea tena kwa Siwatu. Kwa mara ya tatu hawakuja na mchumba, kitu ambacho kilimkasirisha hata Dibwela. Bado Siwatu alionekana hakuwa na furaha. Akili yake ilimuwaza zaidi Bakari kuliko huyo mwingine.

Kimoyomoyo alifurahi mchumba huyo kupata udhuru kwa mara ya tatu ili amkatae.

"Mimi natoka kidogo, unajua yakishaanza haya mambo yako ya uchumba, roho yangu inaniuma, napata presha kwa hiyo natoka zangu kwenda kijiji jirani kwanza nitarudi jioni wakati wakiwa wameondoka, halafu utakuja kunihadithia nini kinaendelea." Alinong'ona Bakari akiwa na Siwatu ndani ili wageni nje wasisikie.

Mbele ya wageni hao Billy na Dausi, walijionyesha kama ni mtu na kaka yake. Ni kama tu kama Dibwela. Kiuhalishia walikuwa wamebadilika.Hawakuishi tena kama kaka na dada kama mwaka mmoja uliopita, walipofanikiwa kuishi miezi mitatu wakilala chumba kimoja.




**"Mpenzi wangu Siwatu." Ilianza barua hiyo "Ni kweli kabisa, hapa Bakari asingependa kuona kitu kama hiki." Akajijibu.**

Sasa hivi walikaa na kuishi kama wapenzi kamili. hakuna aliyeweza kuvumilia tena. Walishaonja asali sasa wanataka kuchonga mzinga.

"Yaani we acha tu, sijui utakuja kusikia kitu gani, maana hawajaja na huyo mchumba mwenyewe, mimi leo nawatolea makavu laivu, kama kaka atakasirika sawa tu."

"Mahari yao waliyotoa je?"

"Watajua wenyewe kaka Dibwela na wazee waliokula." Akajibu.

Bakari akambusu shavuni na kumwambia "Usiwe mtoto mtukutu au mkorofi, wajibu vizuri tu, waridhike waondoke, usionyeshe lolote baya ambalo linaweza kusababisha wahisi kitu, sawa mtoto mzuri?"

"Mmh, na wewe nawe, umekuwa mwanasiasa siku hizi, haya sawa." Akajibu, huku Bakari akitoka na kuwaaga wageni.

Alivyofikiria Siwatu sivyo. Wageni waliokuja walimhabarisha kuwa mchumba angewasili saa 12:00 jioni.

Awali alikuwa anataka kuchukua fursa hiyo kuonyesha kuwa mchumba huyo ni jeuri, hata mapenzi ya kweli na lengo lake ni kwenda kumfanya mtumwa, kwa sababu haikubaliki mara ya tatu mchumba akacha kwenda kujitambulisha.

"Sasa nifanye nini?" Akajiuliza. Kila akijiuliza hakuwa na njia nyingine ya kufanya. Akili ikamruka.

"Tumekuja hapa kama tulivyosema, mchumba anawasilia saa 12:00 jioni leo, saa hizi ni saa sita mchana, kwa hiyo ni masaa sita tu yamebaki. Na sisi tunatoka kidogo, tutarejea mida hiyo kwa sababu tuna mambo mengine ya kufanya, lakini tunawasiliana naye, yeye atakuja kwa gari yake na sisi tuna sehemu tunakwenda tutarudi mida hiyo." Daudi atanabaisha.

"Atapafahamu kweli?" Dibwela aliuliza

"Atakuja na huyo mtu aliyemwambia habari za kuwepo kwa mchumba hapa. yeye anapafahamu vizuri." Daudi akajibu.

Billy alimkabidhi Siwatu bahasha iliyofungwa vizuri. "Bibie huu ni mzigo wake, tumepewa na mchumba wako, mimi sijui wa nini lakini amesema tukukabidhi."

Akapokea huku mikono ikitetemeka. Moyo ulimuenda mbio. Kikubwa hakutamani chochote kutoka kwa hao washenga na mchumba huyo kwa sasa. Aliona ni kama wanampotezea muda. Alitamani hata leo usiku atoroke na Bakari, waende wakaishi mbali na pale. Alikuwa radhi kupoteza nyumba zake mbili na mashamba yake. Hata hivyo mwenzake Bakari yeye anapinga wazo hilo.

*****************************

Akiwa kitandani machozi yanamtoka. Ni dakika 30 tu baada ya washenga kuondoka, aliifungua kwa uangalifu. Mikono yake ilizidi kutetemeka. Hakujua ndani kuna nini na huyo mchumba alimletea nini.

Kuna wakati alidhani ni pesa, lakini baada ya kufungua alikutana na bahasha nyingine nyembamba, ilioonyesha kuwa haikuwa ni pesa bali ni kitu kama nyaraka hivi.

Ni kweli. Yalikuwa ni makaratasi. Akayahesabu. Yalikuwa sita, yaliyoandika kwa wino wa bluu. Mwandishi alionekana ana hati nzuri na iliyopendeza kuisoma.

Akafunga machozi kwa gauni lake. Akili yake sasa ikamtuma asome haraka haraka kabla mpenzi wake Bakari hajamkuta kwa sababu hapendi kuona hali ile ya mwanaume mwingine, haswa mchumba huyo ambaye anataka kumuoa.

"Mpenzi wangu Siwatu." Ilianza barua hiyo "Ni kweli kabisa, hapa Bakari asingependa kuona kitu kama hiki." Akajijibu.

"Mimi ndiyo mchumba wako na ndiye niliyewatuma Billy na Daudi kuja kwenu kwa ajili ya kukuchumbia. Nataka kukwambia mambo machache kabla sijawasili leo jioni huko kwenu. Ni kwa sababu mara mbili nimekosekana huko. Nataka kuja kuona urembo wako mpenzi wangu. Nikubusu ua langu ya rohoni

Kifupi tu mimi naitwa Samson Dau. Hao washenga ambao pia ni wafayakazi wangu wananiita Bosi Mulango.

Kwa muda mrefu nimeishi kwa baba na mama bila ya kuwa na mpenzi. Baba na mama alitaka sana kuniozosha, lakini nilikataa.

Kuna wakati wazazi wangu walitaka kujidhihirisha kama nina tatizo la kiafya kwa sababu hawakuwahi hata siku moja kuniona na mwanamke. Walipojidhihirisha wakaniacha kama nilivyo. Bahati mbaya baba yangu alifariki. Nasikitika amefariki kabla ya kukuoa wewe.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS KULAMBA MIL. 10/-

**Na Hadija Mngwai**

VIONGOZI wa Simba waliotembelea mazoezi ya Timu ya Simba Queens katika Uwanja wa Uhuru juzi, wameahidi kutoa Shilingi milioni 10 kama timu hiyo itaibuka na ushindi leo dhidi ya She Corporate ya Uganda.

Simba Queens imeingia fainali ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake nchini Morroco, itashuka dimbani dhidi ya Waganda hao kwenye uwanja wa Chamazi.

Katika ahadi hiyo, Friends of Simba walitoa kiasi cha shilingi milioni 5 na Simba makao makuu waliahidi kutoa Sh. milioni 5 ikiwa ni hamasa ya kuwawezesha wachukue kombe na kuiwakilisha nchi katika Klabu Bingwa Afrika.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez alisema; "Nawapongeza kwa hatua mliyofikia ya fainali, uongozi upo nyuma yenu, mkapambane muweze kuweka historia ya kuweza kutwaa ubingwa huu kwa mara ya kwanza na kuiwakilisha nchi katika michuano ya kombe la Afrika," alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba Queen, Sebastian Mkoma, alisema watamaliza mechi hiyo ndani ya dakika 45 za kipindi cha kwanza ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa na kuiwakilisha nchi.

"Tumejiandaa vyema Watanzania wengi kwa sasa wanaangalia Simba bila kujali Usimba na Uyanga na badala yake wanaangalia kama wawakilishi wa nchi katika michuano hii, wachezaji wote wapo tayari kifiziki na kiakili kuhakikisha wanashinda mchezo huu na kikosi kipo vizuri na tuna majeruhi mmoja tu," alisema.

"Nimekiandaa kikosi changu kupata matokeo ndani ya dakika 45 za kipindi cha kwanza, hivyo tupo vizuri," alisema Mkoma.



Vijana wakicheza mpira wa kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Azam kujipima kwa Taifa Jang'ombe

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Azam kinatarajiwa kujipima nguvu na Timu ya Taifa Jang'ombe ya Visiwani Zanzibar ikiwa ni maandalizi ya mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jana msemaji wa timu hiyo, Thabit Zakaria alisema mchezo huo ni maandalizi kuelekea mchezo wao dhidi ya Yanga utakaopigwa Septemba 6, mwaka huu, pamoja na mashindano ya kimataifa.

"Tunatarajia kuondoka kesho (leo) kuelekea Visiwani Zanzibar ambapo tutacheza michezo ya kirafiki ili kuwaweka sawa wachezaji wetu," alisema Thabit.

Alisema wanaupa umuhimu mchezo wao na Yanga kwani unatarajiwa kuwa mgumu na wa ushindani.

Msemaji huyo alisema wachezaji wote wamejipanga kupata pointi tatu kwenye mchezo huo.

Kuhusu ushindani wa namba ndani ya kikosi chao alisema ni mkubwa kwani kila mchezaji anapambana apate nafasi ya kupangwa mara kwa mara.

## Polisi Tanzania kuivaa TMA kesho

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Polisi Tanzania kesho inatarajiwa kucheza mchezo wa kirafiki na timu ya TMA kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, John Tamba alisema mchezo huo ni maandalizi ya kujiandaa kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union utakaopigwa Septemba 10, mwaka huu.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri na wale ambao walikuwa majeruhi wameanza kufanya mazoezi mepesi.

"Wachezaji wetu wanaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mchezo huo ambao naamini utasaidia kurekebisha mapungufu ambayo tumeyabaini katika michezo iliyopita," alisema Tamba.

Alisema mchezo wao na Coastal Union utakuwa mgumu na kuahidi kupata pointi tatu.

Alisema amebaini makosa madogo madogo ambayo anaendelea kuyafanyia kazi ili yasijirudie katika mchezo huo.

## Wachezaji Dodoma Jiji wawekwa kitimoto

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, amesema kuwa kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika kikosi chake amelazimika kuzungumza na nyota wake ili kubaini tatizo na kulifanyia kazi.

Dodoma Jiji imeanza vibaya kwenye Ligi Kuu Bara baada ya kufungwa kwenye michezo yote miwili ya awali ambapo anahitaji kujiimarisha zaidi.

Akizungumza na Nipashe, Djuma amesema kuwa, moja ya sababu ya kikosi chake kutofanya vyema kwenye ligi ni kutokana na wachezaji kutozoeana.

"Ligi ina ushindani mkubwa, tumeanza ligi kwa kufanya vibaya na hii inatokana na wachezaji kutoanza mazoezi kwa pamoja," alisema.

"Tunahitaji kujipanga ili kuweza kujiimarisha zaidi, nitakaa na wachezaji wangu kisha nitazungumza na mchezaji mmoja mmoja ili kujua tatizo la kila mmoja lengo likiwa ni kujiweka sawa katika mechi zinazofuata za ligi," aliongeza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PAQUETA OFA MPYA

KLABU ya West Ham imewasilisha ofa mpya kwa kiungo wa kati wa Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 24, baada ya ofa yao ya euro milioni 50 kukataliwa na Lyon. (***Telegraph***)

### CITY WAKATAA KWA SILVA

KLABU ya Manchester City imekataa dau la euro milioni 70, kutoka kwa Paris St-Germain kumnunua kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28. (***Times***)

### FOFANA DAU JIPYA

KLABU ya Chelsea inajiandaa kutoa dau jipya la takriban pauni milioni 75 kumnunua mlinzi wa Leicester, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21. (***Fabrizio Romano***).

### WEST HAM YAKATALIWA

West Ham wametoa pia ofa ya pauni milioni 10 kwa kiungo wa kati wa Ubelgiji, Hans Vanaken mwenye umri wa miaka 30 iliyokataliwa na Club Bruges. (***Evening Standard***)

### ANTONY HAUZWI

KOCHA Mkuu wa Ajax, Alfred Schreuder amesema bado ana imani winga Antony mwenye umri wa miaka 22, hatauzwa kwa Manchester United licha ya dau mpya la hivi punde la pauni milioni 76. (***Metro***)

### ASENSIO APELEKWA MAN

KLABU ya Manchester United imepewa nafasi ya kumsajili winga wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 26 kwa euro milioni 30. (***Telegraph***)

### GAKPO AWINDWA

MANCHESTER United, wanatazamiwa kuwasilisha ofa ya pauni milioni 25 kwa winga wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23. (***Football Insider***)

### PAVARD AWANIWA

KLABU ya Manchester United imetuma ombi la kumnunua beki wa kulia wa Bayern Munich, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 26. (***L'Equipe***)

### TRAPP AIKATAA MAN

GOLIKIPA wa Eintracht Frankfurt na Ujerumani, Kevin Trapp mwenye umri wa miaka 32 amekataa ofa kutoka kwa Manchester United. (***Guardian***)

### LOKONGA ATAKIWA ROMA

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Albert Sambi Lokonga mwenye umri wa miaka 22, yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na Jose Mourinho katika klabu ya AS Roma akitafuta kuchukua nafasi ya Gini Wijnaldum ambaye ni majeruhi. (***AS Roma Live, via Express***)

### ADAMS HAUZWI

KOCHA wa Southampton, Ralph Hasenhuttl amesema mshambuliaji, Che Adams mwenye umri wa miaka 26, hauzwi msimu huu. (***Daily Echo***)

### PALMER ANASAKWA

KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 20 anasakwa kwa mkopo wa msimu mzima na Borussia Dortmund. (***Sun***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE, NEYMAR JR HAWANA UGOMVI – RAIS

**PARIS,** Ufaransa

Avishukia vyombo vya habari kwa kukuza mambo na...

RAIS wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi, amesisitiza kuwa hakuna ugomvi kati ya wachezaji wao nyota Kylian Mbappe na Neymar, kama taarifa zilivyoenea.

Tetesi za kutoelewana kwa wawili hao hapo Parc des Princes zimekuwa zikivuma tangu Paris Saint-Germain iliposhinda 5-2 dhidi ya Montpellier, Agosti 13, ambapo Neymar aliamua kuchukua jukumu la kupiga penalti baada ya Mbappe kukosa ya kwanza.

Wakati wa mchezo huo, Mbappe alionekana kutoridhishwa na wachezaji wenzake wengi, jambo ambalo lilisemekana kuzua taharuki kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na Sergio Ramos, akaingilia kati kuleta amani.

Muda mfupi baadaye, Neymar alionekana kulike Twitter iliyosema kwamba mkataba mpya wa Mbappe na wababe hao wa Ufaransa ulimfanya ajifanye kama "mmiliki wa PSG".

Baada ya droo ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Alhamisi - ambapo Paris Saint-Germain ilitua katika Kundi H na Juventus, Benfica na Maccabi Haifa, Al-Khelaifi alisisitiza kwamba, mpasuko wowote unaodhaniwa kuwa kati ya mastaa wake hao ulikuwa umekuzwa.

"Hapana, hapana. Hakuna tatizo hata kidogo," alisema. "Nadhani ni kweli ... Namaanisha, nadhani ni wewe unayeleta shida haswa, na vyombo vya habari.

"Hakuna tatizo hata kidogo, namaanisha, naweza kugombana na kaka au dada yangu, ni kawaida. Lakini vyombo vya habari kwa sababu ni Kylian Mbappé inakuza mno... wale ni wachezaji wawili marafaki na hawawezi kufanya hivyo."

Baada ya mechi tatu za msimu wa Ligue 1, Paris Saint-Germain ndio timu pekee iliyoshinda mara tatu na imefanya hivyo ikiwa na mabao 17.

"Ni mwanzo mzuri kwetu," alisema Al-Khelaifi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,025,1

MECHI KALI
SOUTHAMPTON
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 3.92
X | 3.74
2 | 1.79

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BENZEMA AMSHINDA BRUYNE TUZO UEFA



**ISTANBUL, Uturuki**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Karim Benzema amechaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa mwaka UEFA msimu wa 2021-22, akimshinda mwenzake, Thibaut Courtois na nyota wa Manchester City, Kevin De Bruyne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliimarisha nafasi yake kuelekea kwenye tuzo za Ballon d'Or mwaka huu kwa ushindi dhidi ya wawili hao, tuzo hiyo ikitolewa wakati wa droo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Istanbul nchini Uturuki, Alhamisi.

Benzema, mfungaji bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na LaLiga msimu uliopita aliwazesha Madrid kutwaa taji hilo, huku alifunga mabao 44 katika michezo 46 katika michuano yote.

Kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti alitwaa tuzo ya kocha bora mbele ya kocha wa Manchester City, Pep Guardiola na Jurgen Klopp wa Liverpool.

Benzema, mwenye umri wa miaka 34 alitajwa miongoni mwa wachezaji 30 wanaowania tuzo ya Ballon d'Or mapema mwezi huu, huku nyota huyo wa muda mrefu wa Madrid akionekana kuwa na nafasi kubwa zaidi.

Benzema alifunga mabao 27 katika michezo 32 ya Madrid iliposhinda LaLiga, na pia alifunga mabao 15 katika mechi 12 za Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati walipobeba kwa mara ya 14, Mei mwaka huu.

Tuzo ya mshindi wa Ballon d'Or mwaka huu inatarajiwa kutolewa Oktoba 17.

# Muller afurahia kupangwa na Lewandowski Ligi ya Mabingwa

**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Muller anasubiri kwa hamu kukutana na mchezaji mwenzake wa zamani, Robert Lewandowski baada ya kupangwa pamoja kwenye droo ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, msimu huu.

Bayern Munich na Barcelona zimepangwa kundi moja kwa msimu wa pili mfululizo, huku Lewandowski akitarajia kurudi pale kwenye dimba la Allianz Arena ikiwa muda mfupi baada ya kuondoka.

Mshambuliaji huyo wa Poland aliweka wazi nia yake ya kuondoka Bayern na kwenda Barca mapema msimu huu wa joto na hatimaye akakamilisha uhamisho wa euro milioni 50 kutua pale Camp Nou.



Kupitia ukurasa wake wa mtandao ya kijamii, Muller alisema: "Ni wakati mzuri tena tutakutana pamoja.

"Lewan-goal-ski, tuonane hivi karibuni mjini Munich...twende, tutikise msimu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Bayern na Barcelona wapo kundi C pamoja na Inter na Milan Viktoria Plzen.

Bayern wameanza kwa kasi msimu mpya licha ya kukosekana kwa Lewandowski, huku Sadio Mane akiongoza safu ya ushambuliaji.

Barcelona walianza kampeni yao mpya kwa suluhu nyumbani dhidi ya Rayo Vallecano, lakini wakapata ushindi wao wa kwanza kwa kuichapa 4-1 Real Sociedad wiki iliyopita, huku Lewandowski akifunga mabao mawili kwa Blaugrana hao.

## HABARI MICHEZO

# 118,259/-

# KOCHA UGANDA AITISHA SIMBA QUEENS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa She Corporate ya Uganda, Hassan Issa, amesema hawatokubali tena kufungwa na Simba Queens mara ya pili kwa sababu wameshawaangalia na kujua upungufu wao na sehemu ambayo wanaitegemea.

Akizungumza kabla ya kuelekea kwenye mechi ya fainali Jumapili ya kusaka tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa kwa Ukanda wa CECAFA, Issa amesema kwenye mechi ya kwanza wachezaji wake walikuwa na hofu ya jina la Simba, lakini sasa wameondoa hofu hiyo baada ya kucheza nao mechi moja kwenye hatua ya makundi.

Ikumbukwe kuwa timu hizo zote zilizoingia hatua ya fainali zimetoka kwenye Kundi B, Simba ikiifunga She Corpotare mabao 2-0 zilipokutana kwenye hatua hiyo na Simba Queens na kuongoza kundi hilo.

"Ni kweli walitufunga kwenye mechi ya kwanza, unajua wachezaji wangu walikuwa wakiogopa jina Simba. Tunajua wana timu nzuri sana, hivyo waliingia na hofu, lakini imeshawaondoka, tunakwenda kucheza mechi ya fainali, unajua fainali siyo mechi kama zingine, inachezwa kimbinu zaidi," alisema kocha huyo.

Alisema, silaha ya Simba Queens ipo kati na mbele, hivyo wamekuwa wakifanyia kazi suala hilo, ambapo watawanyima viungo wao kuwa huru na mpira ili wasiwalishe washambuliaji wao.

"Mimi najua wapo vizuri sana kati na mbele, kwa hiyo ili uwafanye wasicheze vizuri ni lazima uhakikisha viungo wao hawamiliki mipira yenye kuleta madhara," alisema kocha huyo.

She Corporate, ilitinga hatua ya fainali kwa kuichapa CBE ya Ethiopia mabao 2-1, huku Simba Queens ikiivurumisha AS Kigali mabao 5-1.

Bingwa kwenye michuano hiyo atakwenda kuiwakilisha kanda ya CECAFA, kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa zinazotarajia kufanyika mwakani nchini Morocco.



Vijana wakicheza mpira katika kiwanja cha mchanga ndani ya kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Harmoby Tz afyatua 'Uzembe'

**Na Sabato Kasika**

RAPA chipukizi Harmoboy Tz, amefyatua kibao kipya kiitwacho 'Uzembe' ikiwa ni mwendelezo wake wa kuandaa albamu ya kwanza ambayo amepanga kuikamilisha kabla ya mwaka huu haujamalizika.

Chipukizi huyo anayetamani kufanya kazi na Nay wa Mitego, amesema anamini wimbo huo unaweza kumtambulisha akajulikana zaidi kwa mashabiki wa muziki wa kizazi kipya kwa madai kwamba ameupangiliwa vizuri.

"Nilianza na nyimbo za 'Umama, Tunaishi nao, Wanapagawa, Hunitishi na Utapasi Kiatu na sasa nimekuja na 'Uzembe' ambao kwa kweli uko vizuri, unaweza kunitambulisha kutoka anga za muziki wa kizazi kipya," amesema.

Ameongeza kuwa ana ndoto ya kufika mbali kupitia muziki wa kizazi kipya, anaamini ndoto hiyo itatimia kwa kuandaa nyimbo nzuri na kuwashirikisha wasanii wenye majina makubwa.

"Pamoja na kuandaa nyimbo nzuri, msanii ninayechipukia ninatakiwa kushirikisha wasanii wenye majina makubwa ambao ni muhimu kupanda chati kupitia migongo yao," amesema Harmoboy Tz.

Msanii huyo amesema hizo ni mbinu mojawapo zinazotumiwa na wasanii wengi wa ndani na nje ya nchi, ambao wamefanikiwa kuwa matawi ya juu na kwamba hata yeye hana budi kuzifuata ili naye 'atoboe'.

"Nianajua kuwa miongoni mwa kazi za wasanii ni kuelimisha, kuburudisha, kuliwaza na kuikosoa jamii, hivyo ili kufanya vizuri zaidi, ni muhimu kushirikisha wengine kwa ajili ya kupata uzoefu wa kazi," amesema.

Amesema, anajua wapo baadhi ya wasanii ambao hukomaa wenyewe hadi kufikia mafanikio na kwamba njia nyingine ya kufikia huko ni kushirikisha wengine hasa wenye majina makubwa.

"Wito wangu ni kwamba, wasanii ambao wako matawi ya juu washuke chini watuone sisi wadogo zao na kutupa sapoti ili nasi tutoke kama wao, kwani suala la ushirikiano katika muziki ni la muhimu," amesema.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/08/22 | 17:00 | Blackpool vs Bristol City | 2.28 | 3.19 | 3.19 |
| 02. 27/08/22 | 17:00 | Cardiff vs Preston | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 03. 27/08/22 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 04. 27/08/22 | 17:30 | GO Ahead Eagles vs Sparta Rotterdam | 2.33 | 3.53 | 2.84 |
| 05. 27/08/22 | 19:30 | Juventus vs Roma | 2.31 | 3.19 | 3.14 |
| 06. 27/08/22 | 19:30 | Cremonese vs Torino | 2.99 | 3.34 | 2.32 |
| 07. 27/08/22 | 21:45 | Spezia vs Sassuolo | 2.99 | 3.39 | 2.29 |
| 08. 27/08/22 | 22:00 | Lens vs Rennes | 2.44 | 3.36 | 2.76 |
| 09. 28/08/22 | 01:00 | Fluminense vs Palmeiras | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 10. 28/08/22 | 14:00 | Nantes vs Toulouse | 2.40 | 3.27 | 2.88 |
| 11. 28/08/22 | 14:30 | KAA Gent vs Royal Antwerp | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 12. 28/08/22 | 14:30 | Hannover vs Greuther Furth | 2.79 | 3.39 | 2.43 |
| 13. 28/08/22 | 15:15 | FC Lugano vs St. Gallen | 2.45 | 3.49 | 2.69 |
| 14. 28/08/22 | 16:00 | Aston Villa vs West Ham | 2.37 | 3.24 | 2.99 |
| 15. 28/08/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Newcastle | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 16. 28/08/22 | 16:00 | Nice vs Marseille | 2.48 | 3.33 | 2.73 |
| 17. 28/08/22 | 16:00 | Troyes vs Angers | 2.53 | 3.18 | 2.78 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 27 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1278 | Kawasaki Frontale vs Kashima Antlers | 1.81 | 3.49 | 3.83 |
| 13:00 | 3623 | Kashiwa Reysol vs FC Tokyo | 2.21 | 3.09 | 3.09 |
| 14:30 | 1098 | Sunderland vs Norwich City | 3.06 | 3.26 | 2.24 |
| 14:30 | 2496 | Southampton vs Manchester Utd | 3.92 | 3.74 | 1.79 |
| 15:00 | 5260 | Nizhny Novgorod vs Dinamo Moscow | 4.30 | 3.55 | 1.77 |
| 16:30 | 1288 | RB Leipzig vs VfL Wolfsburg | 1.46 | 4.50 | 5.80 |
| 16:30 | 3296 | Hertha BSC vs Borussia Dortmund | 4.19 | 4.19 | 1.66 |
| 16:30 | 3611 | Schalke 04 vs Union Berlin | 2.95 | 3.30 | 2.29 |
| 16:30 | 3868 | Mainz vs Bayer Leverkusen | 2.64 | 3.54 | 2.38 |
| 16:30 | 4178 | Hoffenheim vs Augsburg | 1.44 | 4.70 | 5.80 |
| 17:00 | 1763 | Aberdeen vs Livingston | 1.76 | 3.51 | 4.52 |
| 17:00 | 1901 | Cardiff vs Preston | 2.65 | 2.95 | 2.75 |
| 17:00 | 1921 | Wigan vs Burnley | 3.05 | 3.10 | 2.33 |
| 17:00 | 1944 | Liverpool vs Bournemouth | 1.08 | 8.84 | 22.10 |
| 17:00 | 2647 | Huddersfield vs West Bromwich | 3.74 | 3.34 | 1.95 |
| 17:00 | 2671 | Blackpool vs Bristol City | 2.17 | 3.30 | 3.15 |
| 17:00 | 3025 | Watford vs QPR | 1.88 | 3.35 | 4.00 |
| 17:00 | 4042 | Rotherham vs Birmingham | 1.99 | 3.25 | 3.70 |
| 17:00 | 4200 | Rangers vs Ross County | 1.15 | 7.03 | 15.06 |
| 17:00 | 4471 | Blackburn vs Stoke City | 2.44 | 3.14 | 2.85 |
| 17:00 | 4527 | Chelsea vs Leicester | 1.40 | 4.69 | 6.59 |
| 17:00 | 4938 | Hull City vs Coventry | 2.90 | 3.20 | 2.37 |
| 17:00 | 5116 | Kilmarnock vs Motherwell | 2.61 | 3.16 | 2.66 |
| 17:00 | 5253 | Manchester City vs Crystal Palace | 1.21 | 6.04 | 11.54 |
| 17:00 | 5510 | Brighton vs Leeds | 1.86 | 3.60 | 3.80 |
| 17:00 | 5747 | St Mirren vs Hibernian | 3.27 | 3.06 | 2.26 |
| 17:00 | 5883 | Brentford vs Everton | 1.98 | 3.35 | 3.60 |
| 17:00 | 5894 | Middlesbrough vs Swansea | 1.74 | 3.60 | 4.40 |
| 17:30 | 2320 | GO Ahead Eagles vs Sparta Rotterdam | 2.24 | 3.26 | 3.06 |
| 17:30 | 3988 | Maritimo vs Portimonense | 2.76 | 3.11 | 2.56 |
| 17:30 | 4046 | Fakel vs Spartak Moscow | 4.20 | 3.80 | 1.73 |
| 18:00 | 3907 | AJ Auxerre vs Strasbourg | 3.31 | 3.36 | 2.11 |
| 18:30 | 1414 | Elche vs Real Sociedad | 3.43 | 3.08 | 2.20 |
| 19:00 | 1277 | FC Luzern vs FC Sion | 1.93 | 3.67 | 3.52 |
| 19:00 | 3196 | Jerv vs Bodo Glimt | 10.05 | 6.83 | 1.21 |
| 19:15 | 2037 | OH Leuven vs Oostende | 1.99 | 3.62 | 3.37 |
| 19:30 | 1946 | Cremonese vs Torino | 3.05 | 3.25 | 2.25 |
| 19:30 | 2073 | Juventus vs Roma | 2.39 | 3.02 | 3.02 |
| 19:30 | 2148 | Bayern Munchen vs Monchengladbach | 1.17 | 7.58 | 10.97 |
| 19:30 | 2909 | Arsenal vs Fulham | 1.34 | 4.99 | 7.58 |
| 19:45 | 3722 | Vitesse Arnhem vs Waalwick | 1.68 | 3.75 | 4.60 |
| 20:30 | 3342 | Rayo Vallecano vs Mallorca | 2.07 | 3.18 | 3.68 |
| 21:00 | 4554 | Feyenoord vs Emmen | 1.25 | 5.79 | 9.39 |
| 21:30 | 3358 | Servette Geneva vs Grasshoppers | 1.84 | 3.67 | 3.87 |
| 21:45 | 1138 | AC Milan vs Bologna | 1.33 | 5.00 | 7.80 |
| 21:45 | 3202 | St Truiden vs Mechelen | 2.11 | 3.41 | 3.26 |
| 21:45 | 5572 | Spezia vs Sassuolo | 2.90 | 3.45 | 2.25 |
| 22:00 | 2405 | Lens vs Rennes | 2.52 | 3.38 | 2.62 |
| 22:30 | 4168 | Sporting Lisbon vs GD Chaves | 1.19 | 6.26 | 13.13 |
| 23:00 | 2061 | Almeria vs Sevilla FC | 3.37 | 3.12 | 2.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Agosti 27, 2022
Nipashe

UKURASA 21



## Mbappe, Neymar Jr hawana ugomvi – Rais



Kikosi cha wachezaji na viongozi wa Simba kikiwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Khartoum nchini Sudan jana. **PICHA: SIMBA**

# YANGA SC YAPEWA DOZI YA STAMINA

●●●Nabi aweka ratiba ya mzunguko kwa wachezaji ufukweni na gym kutafuta utimamu wa mwili kwa sababu...

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Nasreddin Nabi, anapambana kutafuta stamina kwa wachezaji wake na kikosi hicho kitaendelea na mazoezi yake kwenye fukwe za Coco, Masaki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi amekiri kuwa hakupata muda mzuri wa kukiandaa kikosi chake kabla ya msimu kuanza hivyo atatumia muda huu ambao Ligi Kuu Bara imesimama kukisuka kikosi chake.

Alisema ratiba yake inabadilika kutokana na jinsi anavyowaona wachezaji wake baada ya mazoezi, huku akibadilisha aina ya programu yake baada ya kumaliza ya Gym wiki hii na sasa wamehamia ufukweni.

"Siku tatu nyuma nilidhani hatutorudi tena gym, lakini jana (juzi) asubuhi tulifanya mazoezi ya utimamu wa mwili jioni tulikuwa uwanjani na leo (jana) asubuhi tulikwenda ufukweni na jioni uwanjani," alisema kocha huyo.

Alisema wachezaji wake wameanza kuelewana kwa kiasi fulani, lakini bado hawajafikia kiwango anachotaka hivyo ataendelea kuyafanyia kazi mapungufu ya kikosi chake.

Nabi alisema malengo yake ni kutetea ubingwa wa Ligi Kuu msimu wa 2022/2023, Kombe la Shirikisho (FA) na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika michezo miwili ya mwanzo ya ligi, Yanga ilishinda 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania kabla ya kuwatandika Coastal Union 2-0.

Mchezo wa mzunguko wa tatu wa ligi, Yanga watacheza na Azam FC, Septemba 6, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuanzia saa 1.00 usiku.

## Simba: Tumejipanga kwa Asante Kotoko, El Hilal

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema wanayatumia mashindano yaliyoandaliwa na Al Hilal kujiandaa na maandalizi ya michezo ijayo ya Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mashindano hayo ni maalum ya timu tatu ambayo yameandaliwa na timu mwenyeji El Hilal.

Wekundu wa Msimbazi hao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika watacheza dhidi ya Big Bullets kwenye Uwanja wa Kamuzu Banda, nchini Malawi.

Simba ipo nchini Sudan ikiwa na wachezaji 16 ikiwaacha nyumbani walioitwa Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' na wengine ni kutoka na matatizo binafsi.

Simba itamenyana na Asante Kotoko ya Ghana kesho Jumapili kabla ya kumalizana na wenyeji, El Hial, Agosti 31, kisha watarejea nyumbani kwa ajili ya mchezo mwingine wa kirafiki dhidi ya mabingwa wa Djibouti, AS Arta Solar.

Akizungumza na gazeti hili juzi wakati wakiondoka, Matola alisema wamefanya mazoezi kwa siku tatu baada ya kumaliza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu na kikosi kipo kwenye hali nzuri na wachezaji wako tayari kwa ajili ya mashindano hayo ambayo yatakuwa kipimo kizuri kwao.

"Mashindano hayo ni mazuri kutokana na aina ya timu tunazoenda kukutana nazo kama Asante Kotoko na wenyeji wetu waliotualika. Ni mazoezi mazuri kwetu kwa ajili ya kwenda kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Matola.

"Tunaenda kukutana na timu bingwa kwenye ligi yao hivyo tunapaswa kujiandaa vizuri, kikubwa napenda kuwahakikishia wana Simba kuwa tunakwenda kupata ushindi," aliongeza.

Naye kiungo mshambuliaji wa Simba, Peter Banda, alisema anaamini mashindano hayo ni muhimu na yataenda kuwaongezea ari ya kujiamini kwenye michezo ya Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Mashindano hayo yatatusaidia hasa benchi la ufundi kupata mwanga wa kikosi na kwenda vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu ikiwamo mchezo wetu wa kimataifa dhidi ya Big Bullets," alisema Banda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002